# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA PILI

**Kikao cha Nne - Tarehe 29 Januari, 2016**

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2015 *(The Annual Report of Energy and Water Regulatory Authority (EWURA) for the Year ended 30th June, 2015).*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kwa Kipindi cha miaka mitano kinachoanzia 2016/2017 - 2020/2021 *(The Framework of the Second Five Year Develepoment Plan 2016/2017 - 2020/2021).*

**MHE. MARTHA J. UMBULLA - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Bajeti kuhusu tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Taifa kwa Kipindi cha Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016) pamoja na Mapendekezo ya Muundo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kwa kipindi cha miaka mitano (2016/2017 - 2020/2021).

**MHE. DAVID E. SILINDE - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI WA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha na Mipango juu ya Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kwa kipindi cha miaka mitano (2016/2017 - 2020/2021).

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. LINA KITOSI - KATIBU MEZANI:** Maswali.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 38

**Tatizo la Maji Kata ya Katumba**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Kata ya Katumba inakabiliwa na tatizo kubwa la maji linalosababisha akina mama wengi kwenda umbali mrefu kutafuta maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufikisha maji katika kata hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Katumba ilikuwa ni kambi ya wakimbizi chini ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi *(UNHCR)* hadi mwaka 2014/2015. Huduma za kijamii zikiwemo maji zilikuwa zinatolewa na *UNHCR*. Ili kutatua tatizo la maji katika kata hii, Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kwa kushirikiana na *UNHCR* imepanga kutekeleza mradi wa maji wa Nduwi Stesheni ili kukidhi mahitaji ya maji kwa wananchi.

Aidha, Halmashauri katika bajeti ya mwaka 2016/2017 imepanga kutenga shilingi milioni 345 ambazo zitatumika kwa ajili ya upanuzi wa mradi huo utakaonufaisha vijiji vya Nduwi Stesheni, Mnyaki A, Mnyaki B, Katumba na Sokoine ambavyo viko katika Kata ya Katumba.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anna Richard Lupembe swali la nyongeza.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa akina mama hao wanatoka mbali na wanaamka usiku wa manane na kwa kuwa wanahatarisha ndoa zao kama katika Kijiji cha Mtambo, Kariakoo, Iwimbi na wako karibu na hifadhi na mara nyingi wanakutana na wanyama wakali kama simba, je, Serikali ina mikakati gani ya kuwasaidia hawa akina mama ili waweze kupata maji karibu na makazi yao kwa sababu wanapata shida sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa Mto Ugala upo karibu sana na Katumba, ni kilometa 20 tu na wananchi wa maeneo hayo wapo takribani 100,000, je, Serikali ina mikakati gani ya kuwasaidia wananchi hao kwa vile wako wengi ili waweze kupata maji kwa urahisi na wepesi zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa haraka wa Serikali, nadhani jana Mheshimiwa Waziri wa Maji alitoa ufafanuzi wakati wa mjadala wa hotuba ya Mheshimiwa Rais kwamba ni kweli changamoto ya maji imeonekana kuwa kubwa. Mheshimiwa Mama Anna naomba nikupongeze sana katika hili maana mara ulipoingia katika nafasi yako umeona kipaumbele cha kwanza ni kushughulikia tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema katika Kijiji cha Mtambo wananchi wanapita katika hifadhi kubwa hivyo lazima wapate huduma ya maji ya haraka. Naomba niseme jambo moja, juzijuzi tulikuwa na semina kubwa na tuliambiwa tulikuwa na awamu ya kwanza ya maji sasa tunaingia katika awamu ya pili ambayo inaanza Januari hii. Mheshimiwa Waziri wa Maji jana alisema katika awamu hii tutaangalia jinsi gani tuweze kutatua matatizo kwenye sehemu zile zenye changamoto kubwa sana ya maji. Mheshimiwa Anna naomba nikuambie Waziri atakapokuja kufanya majumuisho ya Mpango katika suala zima la maji atazungumzia kiuwazi sehemu zenye changamoto tutafanyaje ili mradi tuweze kutatua tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini umezungumzia matumizi ya Mto Ugala, kama Ofisi ya Rais (TAMISEMI) naomba tulichukue ili kuweka mpango mkakati hata ikiwezekana kwa kutumia wataalam wa Halmashauri na Wizara ya Maji tukishirikiana na TAMISEMI kufanya upembuzi yakinifu kuangalia ni jinsi gani mto huu unaweza kutumika kwa ajili ya manufaa ya wananchi wa eneo hilo la Ugala, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa hapo na tafadhali ujitambulishe.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Naitwa Mwalimu Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti. Nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo lililopo Katumba ....

**NAIBU SPIKA:** Samahani Mheshimiwa. Alikuwa amepewa nafasi huyu.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Naitwa Katani Ahmad Katani, Mbunge wa Jimbo la Tandahimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wilaya ya Tandahimba ina vyanzo vingi vya maji ukiwepo Mto Ruvuma na Mahuta lakini bado wananchi wake wanapata tatizo kubwa la maji.

Je, Wizara ina utaratibu gani wa kuhakikisha inaleta mashine ikafunga pale watu wake wakapata maji ya kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli pale Tandahimba kuna mto na ni kweli wana changamoto ya maji. Kama nilivyosema pale mwanzo kila jambo lazima tuwe na mchakato wa upatikanaji wa fedha.

Kwa suala hili katika kikao chetu cha juzi tulifanya maamuzi tukasema lazima Wizara ya Maji na TAMISEMI utendaji wetu wa kazi uwe wa karibu sana. Katika haya nini cha kufanya?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema kila Halmashauri kwanza angalau itenge bajeti ya kuanza kushughulikia yale mambo ya awali mfano kufanya upembuzi yakinifu sehemu ambayo chanzo cha maji kinaweza kupatikana. Hali kadhalika katika mchakato wa bajeti, naomba nizielekeze Halmashauri zote zihakikishe katika bajeti zao ajenda ya maji ni ya msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba ajenda kubwa ya Serikali ni kuhakikisha inatatua tatizo la maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Katani hili ulilolizungumzia Serikali imesikia na inalichukua na lengo kubwa la Mheshimiwa Rais wetu amesema ni lazima tuhakikishe tunamtua ndoo mama, suala hili tutakwenda kulifanyia kazi.

Na. 39

**Hitaji la Hospitali ya Mkoa wa Katavi**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI** aliuliza:-

Mkoa wa Katavi ni moja kati ya mikoa iliyoanzishwa hivi karibuni ili kusogeza karibu na wananchi huduma muhimu za Serikali lakini mkoa huo hauna Hospitali ya Mkoa na Serikali ilishaamua kujenga hospitali hiyo na Serikali ya Mkoa ilishatenga eneo kwa ajili ya ujenzi.

(a) Je, ni lini utekelezaji wa mradi huo utaanza?

(b) Jiografia ya Mkoa wa Katavi ni pembezoni mwa nchi; je, hiyo inaweza kuwa sababu ya kusuasua kwa mradi huo na kupita takribani miaka minne sasa toka Serikali ifanye uamuzi huo lakini hakuna hata dalili chanya kuelekea kukamilika kwa mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimia Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya ujenzi ya Hospitali ya Mkoa wa Katavi yanaendelea ambapo tayari eneo lenye ukubwa wa ekari 243 limepatikana na fidia ya shilingi milioni 468 imeshalipwa kwa wananchi waliopisha maeneo yao kuruhusu ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka 2015/2016, Mkoa umetenga shilingi bilioni moja ambazo zitatumika kuandaa michoro na kuanza ujenzi. Mkoa unasubiri kibali cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili Mshauri Mwelekezi aweze kuanza kuandaa michoro yaani *master plan* na kuendelea na hatua nyingine za ujenzi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kuwa na Hospitali ya Rufaa kwa kila mkoa. Hivyo, Mkoa wa Katavi ni miongoni mwa mikoa mipya itakayojengwa Hospitali ya Mkoa ili kusogeza huduma za afya kwa ajili ya wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapufi swali la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wetu wa Katavi kijiografia upo pembezoni lakini inapotokea shida ya barabara, shida ya

huduma za afya inaufanya mkoa kuendelea kuwa pembezoni. Ninavyofahamu mimi, huduma ya afya kwa maana ya hospitali ni hitaji muhimu. Je, Serikali imejipangaje kulifanya jambo hili kwa haraka ili kunusuru nguvu kazi iliyoko kule kwa kuiepusha na maradhi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, fungu linalotengwa kwa ajili ya uendeshaji wa Hospitali ya Wilaya ni dogo, wananchi wote wa Wilaya ile ya Mpanda ambayo kwa sasa hivi ni mkoa, wanategemea Hospitali hiyo ya Wilaya. Je, Serikali inaisadiaje hospitali ile kwa maana ya kuiongezea bajeti?

**NAIBU WAZIRI WA TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ameuliza Serikali imejipanga vipi kuhakikisha jambo hili linafanyika kwa haraka?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kama nilivyosema awali, Serikali imetenga shilingi bilioni moja katika bajeti ya mwaka huu, tunachosubiri sasa hivi ni kibali cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili mradi kazi hiyo ianze maana huo ndiyo mwanzo. Kazi yoyote haiwezi kufanyika lazima mshauri afanye kazi yake na kibali hicho kitakapotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali nadhani kazi hii itaanza rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mchakato wa bajeti unaondelea sasa katika Ofisi ya Mkoa, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 matarajio ni kwamba hospitali hii itatengewa shilingi bilioni 1.8 ili kuhakikisha watu wa Mkoa huu wa Katavi wanapata huduma ya afya. Umesema miundombinu ya barabara ina changamoto kubwa sana, endapo Hospitali ya Mkoa itakamilika tutawasaidia akina mama. Jambo hili ni la kipaumbele sana katika Serikali hii ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la hospitali yetu ya Mpanda ambayo kutokana na jiografia ilivyo inahudumia wananchi wengi wanaotoka maeneo mbalimbali. Pia inaonekana wazi hata dawa zikipelekwa pale hazitoshelezi na vifaa tiba vina changamoto kubwa. Namshukuru Mheshimiwa Waziri ameweza kupita katika maeneo mbalimbali, ni imani yangu tunakwenda kushughulikia jambo hili. Isipokuwa nawaagiza wataalamu wetu, mara nyingi wamekuwa na kigugumizi kikubwa sana cha kuandaa *data* za wagonjwa wanaotibiwa katika hospitali zao. Niwaagize zile *data sheet* za kusema hospitali inatibu wagonjwa wangapi zikusanywe vizuri. Mwisho wa siku ndiyo hizo *data sheet* ndiyo itakuwa taarifa elekezi ya jinsi gani Hospitali hii ya Mpanda iweze kusaidiwa ili mradi wananchi wapate huduma bora katika maeneo yao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Waziri wa Nchi (TAMISEMI), napenda kujibu sehemu ya pili ya swali, je, Serikali inaisaidiaje Hospitali ya Wilaya ya Katavi katika kuongeza bajeti?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Naibu Waziri, afya ndiyo kipaumbele cha juu katika Serikali ya Awamu ya Tano, kwa hiyo, tutaongeza bajeti katika fedha zinazotoka moja kwa moja Serikalini. Hata hivyo, nimesimama kusisitiza jambo moja, ni lazima tuhakikishe mapato yanayopatikana kutokana na uchangiaji wa wananchi katika kupata huduma za afya yanatumika pia kwa ajili ya kuboresha huduma za afya. Tuwahimize Wanakatavi na wananchi wote wajiunge bima ya afya kwa sababu kadri wananchi wengi wanavyojiunga katika Mfuko wa Bima ya Afya au *CHF*, ndivyo mnavyopata fedha za kuweza kutatua changamoto za bajeti. Tumetoa mwongozo asilimia 60 ya fedha zinazopatikana kutokana na uchangiaji zirudishwe kwa ajili ya kuboresha huduma kama vile kununua dawa, vifaa na vifaa tiba. Kwa hiyo, bajeti haitatosha kwa sababu kasungura siku zote kitakuwa kadogo. Tutumie fedha za makusanyo za Bima ya Afya na *CHF* ili kuweza kutatua tatizo la bajeti ndogo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agness Marwa.

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Hospitali ya Kwangwa ya Mkoa wa Mara iliyopo Musoma Mjini imekuwa ni ya historia kila siku tunaisikia ipo tokea hatujazaliwa hadi leo; na kwa kuwa wanawake na watoto wanapata shida sana na vifo vingi vinasababishwa na umbali wa kutoka Hospitali ya Musoma hadi Mwanza, je, Serikali inaonaje sasa kwa sababu imeshaitengea bajeti Hospitali ya Kwangwa kumalizia suala hilo au kuipa kipaumbele Hospitali ya Kwangwa?

**NAIBU WAZIRI WA TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali imepokea suala zima la Hospitali ya Kwangwa. Maelekezo yetu ni kuhakikisha Hospitali za Wilaya na Mikoa zinafanya vizuri na zile ambazo zina changamoto kama vile miundombinu haijakamilika, changamoto za kibajeti zilizojitokeza katika kipindi cha nyuma kwamba bajeti zimetengwa lakini hazikufika, tunaenda kusisitiza suala zima la ukusanyaji wa mapato, huduma ya afya tumesema ni jambo la msingi ili kila mwananchi apate huduma bora ya afya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Marwa, Serikali imejipanga na katika kipindi hiki tutaangalia bajeti inasemaje katika hospitali hii. Lengo letu

ni kuipa nguvu wananchi wa eneo hilo wapate huduma kwa manufaa ya Serikali yao.

Na. 40

**Kutatua Kero Zinazoikabili Hospitali ya Mkoa wa Tabora**

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH** aliuliza:-

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora inakabiliwa na kero mbalimbali kama vile ukosefu wa madaktari bingwa wa watoto, akina mama, mifupa, na kadhalika; ukosefu wa vifaa muhimu kama vile *ECG machine, CT-Scan, MRI machine,* ukosefu wa huduma za *ICU* pamoja na kwamba lipo jengo zuri lakini halina vifaa vya huduma za dharura:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kutatua kero hizi zinazokabili hospitali hii kwa muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutatua changamoto ya Madaktari Bingwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora, Serikali imewapeleka masomoni Madaktari Bingwa wawili akiwemo Daktari wa Upasuaji na Daktari wa Watoto. Aidha, Mkoa katika bajeti ya mwaka 2015/2016 imeomba kibali cha kuajiri Madaktari Bingwa wanne ili kuboresha utoaji wa huduma ya afya. Kwa sasa hospitali hiyo inatumia Madaktari Bingwa watano kutoka China wanaojitolea ambao wamebobea katika maeneo ya tiba, upasuaji, huduma za uzazi, watoto na huduma ya masikio, pua na koo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa vifaa, Serikali imepanga kusimika vifaa vya kuangalia mwenendo wa afya ya wagonjwa *(patient monitor),* vifaa vya uchunguzi wa tiba vikiwemo *ECG, CTG, Pulse Oxymeter* na *Oxygen Concentrator* katika hospitali zote za ngazi ya mkoa ikiwemo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora. Mpango huu unatarajiwa kuanza mwaka huu wa fedha 2015/2016 na unahisaniwa na Uholanzi kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania. Aidha, Serikali ina mpango wa kuweka huduma ya *MRI* kwenye Hospitali za Rufaa za Kanda na Taifa ambapo kwa mwaka 2015/2016, huduma hii itasimikwa katika Hospitali ya Kanda ya Bugando ambayo inahudumia pia wakazi wa Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Mkoa wa Tabora umeingia makubaliano na Mfuko wa Bima ya Afya *(NHIF),* ili kuweza kukopeshwa vifaa muhimu, hususan kwa ajili ya huduma za dharura *(ICU)*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde swali la nyongeza.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii niweze kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nianze kuipongeza Serikali kwa kutupelekea madaktari wawili kwenda kusoma waje kuwa Madaktari Bingwa kwa sababu hiyo ndiyo njia pekee ya kutusaidia sisi ambao tuko mikoa ya pembezoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile nimhakikishie Mheshimiwa Waziri wale ma-*volunteer* wa Kichina watano anaosema ni Madaktari Bingwa, wanaingia hospitali saa 5.00 na kutoka saa 7.00. Kwa maana hiyo, hawatusaidii ile ni Hospitali ya Rufaa, wagonjwa wanaingia ndani ya masaa 24. Kwa hiyo, wale Madaktari wa Kichina watano anaowasema hawatusaidii ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikisema Bungeni hapa toka 2011 nikidai Madaktari Bingwa wa Mkoa wa Tabora, akina mama wanapata vifo vingi vya uzazi, watoto wetu wanakufa kwa sababu hatuna Madaktari Bingwa, vijana wetu madereva wa bodaboda wanavunjika miguu, hatuna Madaktari Bingwa wa Mifupa. Hii imekuwa kero kubwa kwetu sisi Wabunge ndani ya Mkoa wa Tabora na nimekuwa nikilisemea hilo kwa muda mrefu toka 2011 naingia hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri hajanijibu vizuri, ana mkakati gani wa kutuletea Madaktari Bingwa ndani ya Mkoa wa Tabora?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeomba vibali miaka 10 iliyopita lakini hatujapewa kibali cha kuajiri Madaktari hao. Naomba anijibu ana mkakati gani wa kutuletea Madaktari Bingwa katika Mkoa wa Tabora kwa sababu watu wanakufa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kuhusiana na vifaa. Niipongeze Serikali kwa mkakati wake mzuri wa kusema kwamba Bima ya Afya itatukopesha na tupate vifaa ndani ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora. Hospitali ni ya siku nyingi, haina vifaa vyovyote, watu wanaendelea kufa. Hata hivyo, nimesema hatuna huduma ya *ICU* pale Tabora…

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko tayari kufuatana nami kwenda Tabora kuangalia changamoto zilizopo katika Hospitali ya Rufaa?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane na tuheshimiane. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, usimuone Mheshimiwa Munde ana-*rap* sana ni kwamba ameguswa na jambo hilo na ndiyo maana nimesema kwamba Serikali imepeleka madaktari kwa ajili ya kwenda kubobea katika maeneo hayo na lengo kubwa na mahsusi ni kwa ajili ya Mkoa wa Tabora, hili ni jambo moja kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafahamu fika, wiki chache zilizopita nilifika Mkoani Tabora pale. Nilienda katika Kituo cha Afya cha Bukene na Itobo, kote kuna vifaa vya upasuaji vinataka wataalam. Hata katika kipaumbele chetu tumesema suala la Mkoa wa Tabora lazima liwe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana wataalam wetu, mara nyingi sana hospitali zilizoko pembeni madaktari wanaona ni tabu sana kwenda kwenye maeneo hayo. Sisi sasa hivi tumejipanga, lengo letu ni kuelekeza wataalam kwenye maeneo yote ya pembezoni na kuhakikisha kwamba wataalam wanaosomeshwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaenda kuwahudumia Watanzania.

Suala la vifaa nimesema pale mwanzo na Waziri wa Afya na yeye analizungumza mara nyingi sana kwamba suala la vifaa kuna utaratibu maalum. Naomba niwaambie, kuna mchakato mkubwa sana wa hivi vifaa mwisho wa siku Hospitali zote za Kanda na Mikoa zifungiwe vifaa maalum ili mradi akina mama na wagonjwa mbalimbali waweze kuhudumiwa. Huu ni mpango mkakati wa Serikali na unaanza mwaka huu. Kwa hiyo, dada yangu Munde usihofu, mimi mtani wako umesema tuongozane, nitaongozana na wewe Mungu akijalia. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Devotha Minja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Devotha Minja, naomba ukae. Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi (TAMISEMI), napenda kuongeza kidogo ufafanuzi katika suala la uhaba wa watumishi *especially* Madaktari Bingwa, nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba tumefanya tathmini ya uhaba wa watumishi katika sekta ya afya, *especially* Madaktari na Madaktari Bingwa. Tumebaini mikoa tisa ina uhaba mkubwa ikiwemo Tabora, Simiyu, Katavi, Geita, Shinyanga, Rukwa na Singida.

Kwa hiyo, kipaumbele cha ajira za Madaktari Bingwa katika mwaka huu tunatoa katika mikoa hiyo tisa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Munde na Waheshimiwa Wabunge wengine wote ambao mnatoka katika hiyo mikoa tisa tutawapa kipaumbele kwa sababu mnao uhaba wa wataalam chini ya 52%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumekusudia kufanya zoezi moja kugumu sana. Tunataka kuondoa tatizo la Madaktari Bingwa wataalam kurundikana katika mkoa mmoja na kuiacha mikoa ya pembezoni, kwa hiyo, tunataka kuangalia mgawanyo.

Waheshimiwa Wabunge mtuvumilie tutakapoendesha zoezi hili gumu mkasema huyu naomba umbakize, mwanamke wa Rukwa, Katavi, Njombe, Simiyu, ana haki ya kupata huduma za Daktari Bingwa kama mwanamke wa Dar es Salaam. Kwa hiyo, tunataka kuendesha zoezi la *redistribution,* tuwatawanye madaktari waende mikoani wakatoe huduma ili wanawake wa huko wapate huduma nzuri kama wanawake wa Dar es Salaam, Arusha na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Devotha Minja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Kwa kuwa matatizo ya ukosefu wa huduma katika Hospitali za Mkoa wa Morogoro hayana tofauti na matatizo ya Mkoa wa Tabora. Mkoa wa Morogoro una Hospitali ya Rufaa ambayo inatoa huduma katika wilaya zake zote lakini cha kusikitisha hospitali hiyo haina huduma ya *X-ray.* Huduma ya *X-ray* iliyopo ni ya zaidi ya miaka 20 iliyopita hali ambayo inawalazimu wagonjwa waliolazwa hata wodini kwenda kupata huduma za *X-ray* nje ya hospitali hiyo katika Hospitali za Mzinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inapeleka huduma hizo za *X-ray* katika Hospitali hii muhimu ya Rufaa ambayo inategemewa na wananchi wa Mkoa wa Morogoro?

**NAIBU WAZIRI WA TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, hiki kilio tumekisikia na tunajua Morogoro ni *center*. Ukisema huduma ya *X-ray* pale Morogoro hakuna wakati tukijua Morogoro ni muungano wa barabara mbili, inayotokea Dodoma na ile inayotokea Iringa, na katika njia moja au nyingine kama kesi za ajali za magari lazima mgonjwa moja kwa moja atapelekwa katika Hospitali ya Mkoa. Sasa kama changamoto hii ni kubwa kiasi hiki, naomba niseme katika zoezi letu la kupeleka vifaa vya upimaji tutahakikisha Morogoro inapewa kipaumbele. Naomba aiamini Serikali yake itaenda kufanya kazi hiyo haraka iwezekanavyo.

Na. 41

**Sera Mpya ya Elimu ya Mwaka 2014**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Sera Mpya ya Elimu ya mwaka 2014 inatambua upatikanaji wa elimu ya msingi bure; lakini Serikali imeshindwa kupeleka ruzuku ya shilingi 10,000 kwa kila mwanafunzi wa shule za msingi za umma na shilingi 25,000/= kwa kila mwanafunzi wa shule za sekondari za umma:-

Je, Serikali inaweza kuweka mchanganuo wa jinsi gani itakavyoweza kutekeleza Sera ya Elimu ya mwaka 2014 kwa kutoa elimu bure bila kuathiri ubora wa elimu?

**NAIBU WAZIRI WA TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malopo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli fedha za uendeshaji wa elimu *(capitation)* zikiwemo shilingi 10,000/= kwa wanafunzi wa shule ya msingi na shilingi 25,000/= kwa wanafunzi wa sekondari zilikuwa hazipelekwi kwa ukamilifu. Kwa sasa Serikali imeamua kuanzia Januri, 2016 wanafunzi wote walioandikishwa darasa la kwanza na wale walioandikishwa kidato cha kwanza pamoja na wale wanaoendelea na shule gharama zilizokuwa zinagharimiwa na wazazi au walezi kwa kulipia ada na michango mbalimbali sasa zitalipwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia Serikali imetenga shilingi bilioni 131.4 ikiwa ni fedha za ruzuku ya uendeshaji wa shule, chakula, mitihani na fidia ya ada. Fedha hizo zitapelekwa moja kwa moja shuleni kutoka Hazina kwa wastani wa shilingi bilioni 18.77 kila mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizo zinahusisha shilingi 10,000/= kwa wanafunzi wa shule ya msingi kwa mwaka, shilingi 25,000/= kwa mwanafunzi wa sekondari kwa mwaka, shilingi 1,500/= kwa kila mwanafunzi kwa shule za msingi na sekondari kwa ajili ya chakula, fidia ya ada ya shilingi 20,000/= kwa wanafunzi wa kutwa na shilingi 70,000/= kwa wanafunzi wa bweni kidato cha kwanza hadi cha nne kwa mwaka. Tayari Serikali imeshapeleka shilingi bilioni 18.77 kwa mwezi Januari, 2016.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malapo swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kutoa masahihisho, Naibu Waziri wakati anajibu aliniita Malopo naitwa Malapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu hayo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, je, Serikali iko tayari sasa kuwaambia wananchi kuwa haiko tayari kutekeleza Sera ya Elimu Bure kwa maana halisi ya Kiswahili ya neno bure isipokuwa elimu inayotolewa sasa ni ya kuchangia gharama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, nini wito wa Serikali kwa wananchi kuhusu sera hii ili kuwawezesha walimu kufanya kazi yao bila kero kutoka kwa wazazi wanaofikiri hawawajibiki kulipa pesa yoyote kwa ajili ya elimu hiyo kwa watoto wao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante. Kwanza naomba radhi kwa kukosea jina la Mheshimiwa Mbunge ni Malapo na nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala kwamba Serikali iseme haina nia ya dhati katika suala zima la elimu bure, ndugu zangu naomba niwaambie, kama sisi ni mashahidi wa kweli vijana wengi waliokuwa wanaenda sekondari walikuwa wanashindwa kulipa hizi gharama za kawaida. Hata wale waliokuwa wanaanza elimu ya msingi mnafahamu wazazi wengi sana wanashindwa kulipa zile gharama za awali ili mtoto wake aweze kujiunga na shule na ninyi wenyewe ni mashahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi juzi kupitia vyombo vya habari wazazi wanakiri kabisa kwamba suala hili limewasaidia kwa kiwango kikubwa vijana wao kwenda shule. Hata *turn over* katika shule zetu imekuwaje? Hata madarasa wakati mwingine shule zinahemewa kwa sababu wazazi wote ambao mwanzo walikuwa wanakwazika na gharama hizi sasa wanapata fursa ya kuwapeleka watoto wao shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tukiri kwamba Serikali katika hili imefanya juhudi kubwa sana. Naamini jambo lolote lazima lina changamoto zake, hizi changamoto ndogo-ndogo ni kwa ajili ya kuboresha ili mradi mpango uende vizuri lakini dhana ya Serikali imekamilika na inaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya pili, wito wa Serikali Walimu wasibughudhi wazazi, nadhani tumeshasema wazi na Waziri wangu jana alilisema wazi kwamba jambo kubwa elimu hii ni bure. Hatutarajii mwalimu awazuie watoto kwenda shule kwa kuzusha mchango wake mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili tumesema tutakuwa wakali sana kwani lengo kubwa ni mtoto wa Kitanzania aweze kupata elimu ya shule ya msingi na ya sekondari mpaka *form four.* Lengo ni kwamba kila mwanafunzi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania apate fursa ya uongozi na mikakati ya Serikali ya Awamu ya Tano.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuongezea majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri wa TAMISEMI kutokana na maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Malapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali imefanya jitihada kubwa katika suala hili la elimu bure, lakini inasikitishwa kwamba wenzetu walihoji fedha hizi zimetoka wapi kwenye bajeti na leo fedha hii iliyotolewa kwa ajili ya kusaidia jamii maskini watoto wao waende shule wanahoji tena hiyo bure gani, ni mkanganyiko ambao haueleweki. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme tu, katika kila shule za msingi za kutwa tutapeleka kila mwezi shilingi 600/= kwa kila mtoto kwa ajili ya uendeshaji. Kwa shule za sekondari za kutwa tunapeleka kwa kila mwezi shilingi 3,540.57/= kwa kila mtoto kwa ajili ya uendeshaji wa shule. Kwa wale wa bweni tunapeleka shilingi 7,243.39/= kwa kila

mwezi. Fedha hizi zikijumlishwa uwezekano wa kuendesha elimu upo pamoja na changamoto zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ninavyozungumza kutokana na mpango huu wa elimu msingi bila malipo pale ambapo tulitegemea wajiandikishwe watoto 80 kuanza darasa la kwanza wamejiandikisha 240; pale tulipotaka wajiandikishe watoto 180 wamejiandikisha karibu 700 na hiyo ni Dar es Salaam tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako baadhi ya maeneo uwezekano tu wa kuwapokea watoto hawa ni mgumu kwa sababu wazazi maskini wameona mpango huu ni muhimu kwao na umewasaidia sana.

Kwa hiyo, kuubezabeza hapa ni kwenda kinyume kabisa na wananchi ambao wanaona mpango huu umewasaidia na kwa hakika kusema kweli unalisaidia Taifa. Tupingane katika mengine lakini kwenye jambo zuri tutiane moyo kama Watanzania. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa pale nyuma na jitambulishe tafadhali.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona, naitwa Mwalimu Mussa Ramadhani Sima, Mbunge wa Singida Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika huu mpango wa Serikali wa kutoa elimu bure, napenda kufahamu Serikali ina mpango gani sasa kuboresha maslahi ya walimu kwa mpango utakaoitwa elimu bure na maslahi bora kwa walimu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua umuhimu wa ualimu, lakini vilevile tunatambua umuhimu wa watumishi wote wa umma. Lakini kwa kutambua umuhimu huo wa walimu kama Serikali, kwa miaka takribani nane tumeshapandisha takribani asilimia 160 ya mshahara wa walimu. Ukiangalia hivi sasa mwalimu wa chini kabisa anapata shilingi 419,000/=, na wa juu anapata shilingi 719,000/=. Tunatambua bado mazingira ya kuishi gharama ni kubwa na wanahitaji kuongezewa kipato na tutafanya hivyo kwa kadri hali ya uchumi itakavyokuwa ikiruhusu.

**NAIBU SPIKA:** Tuendelee, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Kasuku Samsom Bilago, Mbunge wa Buyungu aulize swali lake.

Na. 42

**Mwajiri wa Walimu nchini**

**MHE. KASUKU S. BILAGO** aliuliza:-

Kifungu cha 3 cha Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, na Kifungu cha 1(26) cha Kanuni za Kudumu za mwaka 2009 vinatoa tafsiri ya neno mwajiri kuwa ni mtu au taasisi ambayo mtumishi wa umma anaingia naye mkataba wa ajira na kumlipa mshahara.

Je, kwa kuzingatia tafsiri hiyo, mwalimu ambaye ni mtumishi wa umma, mwajiri wake ni nani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kujibu swali la Mheshimiwa Mwalimu Kasuku Samson Bilago Mbunge wa Jimbo la Buyungu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwajiri wa watumishi wote wa umma wakiwemo walimu ni Serikali ambayo ndiyo inakusanya mapato na kulipa mishahara ya watumishi wake. Hata hivyo, Serikali imekasimu madaraka kwa mamlaka mbali mbali kama ilivyoainishwa kwenye kifungu cha 6(1) cha sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutungwa kwa sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu, sheria namba 25 ya mwaka 2015, Idara ya Utumishi wa Walimu ndiyo ilikuwa Mamlaka ya Ajira na nidhamu kwa walimu wote walio kwenye Utumishi wa Umma. Baada ya kutungwa kwa sheria hiyo ya Tume ya Utumishi wa Walimu namba 25 ya mwaka 2015, iliyoanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu.

Tume hii sasa ya Watumishi wa Walimu pamoja na majukumu mengine itakuwa Mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa Walimu wa shule za msingi na sekondari walioajiriwa na Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimwa …

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika samahani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza jukumu la kuwa mwajiri, Serikali huingia Mikataba ya Ajira na kulipa mishahara ya Walimu kupitia mamlaka za Serikali za Mitaa wanakofanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bilago swali la nyongeza

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Waziri mwenyewe amekiri katika majibu yake ya swali la msingi kwamba ajira ya walimu imekasimiwa kwenye mamlaka zingine, na mamlaka zilizokasimiwa ajira za walimu ndizo zimesababisha matatizo makubwa ya walimu, walimu kutopanda madaraja kwa wakati, walimu kutolipwa mishahara mizuri na walimu kutolipwa madai yao kwa muda mrefu sana.

Je, Waziri yuko tayari hii Tume iliyoundwa namba 25 ya mwaka 2015 iwe na mamlaka kamili ya kuwaajiri na kulipa mishahara bila kukasimiwa kwenye mlolongo wa vyombo vingine?

Swali la pili, kwa kuwa matatizo yaliyosababishwa ya walimu nchini yametokana na mfumo kwa kukasimu mamlaka ya ajira ya walimu kwa vyombo vingine vingi kuanzia Katibu Kata, Mratibu, *TSD,* Utumishi, Hazina na kadhalika, vyote vinavyoleta usumbufu kwa ajira ya mwalimu na maslahi yake kupotea.

Je, Serikali iko tayari kuwahudumia walimu kwa dharura kabisa kulipa madai yao yanazidi shilingi bilioni 20 kwa dharura ya haraka ili walimu hao waweze kufanyakazi kwa moyo? Asante

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwalimu Bilago ametaka kujua kama Serikali iko tayari kuipa Tume ya Utumishi ya Ualimu mamlaka kamili ya kulipa mishahara. Niseme tu kwamba ukiangalia katika kifungu cha 5 kinachoanzisha Tume hii ya Utumishi wa Walimu, Mamlaka kwa Tume hii ni Mamlaka ya ajira. Bado suala zima la kulipa mishahara kama ilivyo Kanuni ya Utumishi wa Umma na kama wanavyolipwa watumishi wote wa umma itabaki katika Serikali. Lakini ukiangalia kama Mamlaka ya Usimamizi kwenye Serikali za Mitaa, ambao ndio wanaendesha na wenye shule uko chini, wao wanachokifanya ni kulipa tu mishahara kwa kuwa wao ndiyo mamlaka ya usimamizi, kwa hiyo tutaendelea hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba pamekuwa na changanmoto ambazo tunazitambua kwa kuanzisha Tume hii tunaamini sasa kwa kuwa ni Tume ambayo inajitegemea, maana ukiaangalia huko awali Idara ya Walimu ilikuwa chini ya Utumishi wa Umma, lakini Tume hii mpya ambayo

tunayoianzisha itakuwa ni Tume inayojitegemea na tunaamini sisi kama Serikali kwa kuwa tumejipanga kuiwezesha kwa rasilimali fedha, kuiwezesha kwa rasilimali watu na vitendeakazi mbalimbali tunaamini changamoto mbalimbali ambazo zilijitokeza basi zitaweza kutatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge aweze kuwa na imani, tuweze kuanza Tume hii halafu tuone mambo yatakavyojitokeza lakini sisi kama Serikali tuko tayari kuiwezesha Tume hii kwa hali na mali. Ukiangalia katika mahitaji ya kibajeti yaliyobainishwa ni takribani shilingi bilioni 75, wakati ukiangalia ni ilipokuwa ni Idara ya Utumishi wa Walimu walikuwa wanategemea bajeti yao kutoka katika Tume ya Utumishi wa Walimu, ndiyo maana changamoto mbalimbali za kupandishiwa mishahara, changamoto za kupandishwa madaraja na mambo mengine yalikuwa zinajitokeza. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge aiamini Serikali, tuipe nafasi Tume iweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la pili kuhusiana na madeni ya walimu, kama nilivyoeleza jana. Ni kweli madeni ya walimu yako katika kiwango cha juu, takribani shilingi bilioni 42, lakini hivi sasa tunachokifanya ni kuhakiki madeni haya. Nilitoa angalizo, yako madeni au madai yanayowasilishwa ambayo unajikuta yana mapungufu fulani, yako ambayo unajikuta hayana nyaraka mbalimbali za kiutumishi. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Serikali tutajitahidi kuhakikisha kwamba tunalipa madeni haya haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sasa kupitia Bunge lako Tukufu, kwa kuwa mfumo wetu wa *Human Capital Management System* uko katika Halmashauri mbalimbali, niwaombe Waheshimiwa Wabunge ambao nao ni Madiwani katika Halmashauri husika waweze kufuatilia madeni haya, yako kiasi gani kwa mwezi husika, mwezi unaofuata unatarajiwa kulipa kiasi gani, lakini vilevile endapo kuna madai ambayo yamerudishwa changamoto ni nini, waweze kutusaidia.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na matatizo makubwa ambayo wanayo Walimu na nia ya Serikali kuyatatua ipo kada nyingine ambayo ni kama inasahaulika na hii ni kada ya Wakaguzi wa Elimu. Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba kada hii nayo inatazamwa ili kwa pamoja na kwa kushirikiana na walimu waweze kusaidiana katika kuboresha elimu ya watoto wetu katika nchi yetu?

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Serikali tayari imeshaanza mkakati wa kuboresha ukaguzi wa shule na sasa hivi hata kuna muundo mpya wa wakaguzi, ambapo hata jina la ukaguzi limebadilishwa, wanaitwa Wathibiti wa Ubora wa Elimu, na yote hii ni katika lengo la kuhakikisha kwamba tunaimarisha zaidi ukaguzi wa shule kwa kuangalia wakaguzi wanavyoweza kufanya kazi zao kwa kufanisi zaidi. Ukaguzi umeimarishwa mpaka katika ngazi za Wilaya, na huu muundo unaendana pia na maslahi bora kwa wakaguzi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haonga swali fupi.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Kwa kuwa walimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi walisimamia mtihani wa kidato cha Nne mwaka jana 2015 hawajalipwa fedha zao. Je, Serikali haioni ni mwendelezo wa kuwanyanyasa walimu na kuwaonea?

**NAIBU WAZIRI (TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika asante. Mheshimiwa Pascal juzi wakati anajadili hapa nadhani alizungumzia suala la Mbozi, na ofisi yetu inalifanyia kazi kushirikiana na Hazina na katika mchakato tunaoondoka nao walimu wote ambao malipo yao yalikuwa bado hayajakamilika basi yataweza kusawazishwa na jambo hili likaweza kukaa vizuri, Serikali inafanyia kazi jambo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tuendelee, swali linalofuata Mheshimiwa Abdalah Mtoka Mbunge wa Temeke aulize swali

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, umeruka swali.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge jina lilikuwa limekosewa, Mbunge wa Temeke anaitwa Abdallah Mtoka siyo Mtulia. *(Kicheko)*

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, jina langu naitwa Abdallah Ally Mtolea

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, umeruka swali.

**NAIBU SPIKA:** *Okay*, samahani, swali namba 43 Mheshimiwa Desderius John Mipata Mbunge wa Nkasi Kusini. Lakini pia nisaidiwe majina ya hili Swali namba 44 maana nimeletewa ujumbe kwamba mwenye swali ni Mbunge wa Temeke na siyo Mbunge wa Kinondoni, niletewe hizo taarifa tafadhali. Mheshimiwa Mipata uliza swali tafadhali.

Na. 43

**Ahadi za Mawasiliano ya Simu za Mkononi – Nkasi Kusini**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Wakati akiwa Makao Makuu ya Jimbo la Nkasi Kusini, Makamu wa Rais wa Serikali ya Awamu ya Tano, aliwaahidi wananchi wa Jimbo hili mawasiliano ya simu za mkononi kwa Kata nne za mwambao wa Ziwa Tanganyika ambazo ni Ninde, Wampembe, Kizumbi na Kala; je, ni lini utekelezaji wa ahadi hiyo utafanyika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata wa Nkasi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutekeleza sera ya kuzipatia huduma ya mawasiliano ya simu Kata zenye uhitaji ili kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa wananchi, wakiwemo wa Jimbo la Nkasi Kusini. Katika mwaka wa fedha wa 2015/16 Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote *(UCSAF)* imetenga jumla ya dola za Kimarekani 199,850 kwa ajili ya upelekaji wa mawasiliano katika Kata ya Ninde katika Awamu ya Pili A ya mradi huo. Kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom Tanzania ndiyo iliyopewa zabuni ya kupeleka mawasiliano katika Kata hiyo. Mradi ulianza kutekelezwa kuanzia mwezi Aprili, 2015 na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata za Wampembe, Kizumbi na Kala, zimejumuishwa katika mradi wa mawasiliano vijijini Awamu ya Kwanza A *(Phase I A)* wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na maandalizi ya ujenzi wa mnara yanaendelea chini ya kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom Tanzania. Kwa sasa Vodacom wanawaandaa wakandarasi wa kutekeleza mradi huo ambao ujenzi wake umepangwa kukamilika mwezi Juni, 2016.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mipata swali la nyongeza

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, katika Bunge la Kumi nilitumia muda mwingi sana kufuatilia na kuuliza maswali juu ya upelekaji wa huduma hii kwenye Kata hizi za mwambao na sababu kubwa ni kwamba Kata hizi ni za mpakani, zina changamoto myingi zikiwepo changamoto za kiusalama pamoja na usafiri,

barabara zake hazipitiki vizuri. Majibu yaliyokuwa yanatolewa na Serikali hayana tofauti na haya, na sasa hivi Serikali kama imejichanganya kidogo. Mara ya mwisho walikuwa wanasema Halotel ndiyo wangeweza kupeleka mawasiliano kule, sasa wanakuja na msimamo wa Vodacom jambo ambalo litawachanganya wananchi kikamilifu, na nilikuwa juzi Kata ya Ninde ambako wanasema utekelezaji umekwishaanza, hakuna dalili zozote zaidi ya kwenda kuonyeshwa *site* basi. Vilevile Wampembe hakuna kitu kinachoendelea, kwa hiyo nina mashaka majibu yamekuwa ni yale yale, ninaiomba Serikali ihakikishe kwamba inapeleka mawasiliano haya kama inavyoahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasizoee kuahidi wanieleze leo ni miujiza gani wataifanya iwe tofauti na ahadi walizokuwa wanazitoa wakati ule?

Swali la pili, katika Jimbo langu pia hasa Kata ya Isale. Kwanza niishukuru Serikali kwa kupeleka mawasaliano Kata ya Kate, kuongeza usikivu na hatua nyingine inayoendelea kwenye Kata ya Sintali. Kata ya Isale yenye vijiji vya Msilihofu, Ntuchi na Ifundwa, usikivu siyo mzuri, na nilipata kuuliza hapa pia nikaelezwa kuna hatua na kampuni imepewa kazi ya kuboresha mawasiliano katika eneo hilo, nataka kujua ni lini kazi hiyo itakamilika? Asante.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba ajue hii ni Serikali ya awamu ya Tano, ni Serikali ya kasi, ni Serikali ya hapa kazi tu. Ahadi tuliyokupa imezingatia *commitment* iliyotolewa na mfuko huo tunaoongelea *UCSAF*. Kwa hiyo ninakuahidi, kama ulivyosisitiza mwenyewe na mimi narudia kwamba ifikapo mwezi Juni 2016, Kata hizo tatu mawasiliano yatakuwa yamefikishwa na atakayefikisha ni Vodacom Tanzania. *(Makofi)*

Kuhusu swali lako la pili, kama unavyoniona huwa napenda kusema kitu ambacho kina takwimu. Swali hili ni jipya kwangu na nakuhakikishia baada ya saa tisa alasiri tuonane nitakuwa nimewasiliana na watu wa *UCSAF* nikupe majibu sahihi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante. Kwa jina naitwa Boniphace Mwita ni Mbunge wa Jimbo la Bunda na ieleweke hivyo, mdogo wangu Ester Bulaya ni Mbunge wa Bunda Mjini.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya Jimbo la Bunda yanafanana na matatizo ya Nkasi, kuna Kata ya Unyari, ambayo ina vitongoji vyake na maeneo yake, ambavyo ni Nyamakumbo, Manangasi, Magunga, na Nyamatutu, na kijiji

cha Kihumbu vitongoji vyake na Kihumbu na Mwimwalo vina tatizo lile lile la kutokuwa na mawasiliano, na kwa kuwa maeneo haya yana wakulima wengi na wafugaji wengi, na kwa kuwa wakulima hawa wako kwenye hali hatari ya tembo.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kuna umuhimu sasa wa kupeleka mawasiliano maeneo hayo ili wajiokoe na hali ya ulinzi wake na pia kwa mawasiliano ya kawaida?

Kwa kuwa wananchi hao wamechoka kuahidiwa na leo wamekuja hapa Bungeni kuonana na Waziri kuhusiana na maeneo yao hayo.

Je, Waziri yuko tayari kuonana nao leo? *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri jibu swali moja.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumhakikishia Mbunge kwamba nitakuwa tayari ofisini tuonane tu-*discuss* masuala yote aliyoyaongelea na tumpe takwimu sahihi.

Na. 44

**Malipo ya Fidia kwa Nyumba Zilizovunjwa Kupitisha Upanuzi wa Barabara ya Kilwa**

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA** aliuliza:-

Kufuatia upanuzi wa barabara ya Kilwa mwaka 2002 wapo wananchi 80 waliolipwa maeneo ya Kongowe mwaka 2008 na wengine 111 walilipwa baada ya hukumu ya shauri lililofunguliwa na ndugu Mtumwa.

Je, Serikali itakamilisha lini malipo ya fidia ya nyumba zote zilizobomolewa kupisha upanuzi wa barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea, Mbunge wa Temeke kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali hili linaulizwa mara saba na Wabunge mbalimbali wa Temeke ikiwa ni pamoja na Wabunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Dar es Salaam. Ninawaombeni Waheshimiwa Wabunge tunapotoa majibu ni muhimu tukawaeleza wananchi majibu hayo na tukienda nje ya hapo

tutakuwa tunarudia rudia na sisi wengine hatujisikii vizuri tunaporudia kutoa majibu .

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uwepo wa wananchi wanaodai fidia kutokana na nyumba zao zilizokuwa zimejengwa ndani ya eneo la hifadhi ya barabara ya Kilwa ambayo ilibomolewa mwaka 2002 kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na. 167 ya mwaka 1967.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nyumba hizo zilijengwa ndani ya eneo la hifadhi ya barabara na hivyo kukiuka Sheria ya Barabara namba 167 ya mwaka 1967, Serikali haina mpango wa kuwalipa fidia wamiliki wa nyumba hizo kwa kuwa hawastahili kulipwa fidia.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kutokana na majibu haya yasiyokuwa na tija kwa wananchi wa Temeke yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo yanatushawishi sasa kwenda kuidai haki yetu Mahakamani, naomba niulize maswali matatu ya nyongeza. *(Kicheko)*

Samahani naomba niulize maswali mawili ya nyongeza moja lina sehemu (a) na (b).

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtolea nadhani utakuwa umeziangalia Kanuni kuhusu maswali, ukiuliza swali moja lenye (a) na (b) kwa sababu ni nyongeza utakuwa umeshauliza hayo mawili, tafadhali.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kilwa ilijengwa chini yakiwango, na Serikali ilimwamulu mkandarasi airudie kwa gharama zake mwenyewe. Ujenzi huo wa chini ya kiwango ni pamoja na mitaro iliyo pembezoni mwa barabara hiyo, mvua zilizonyesha tarehe 14 na tarehe 15 Disemba, mitaro hiyo ilishindwa kuyabeba maji vizuri na ikapasuka ikapeleka maji kwenye makazi ya watu maeneo ya mtaa wa Kizinga katika Kata ya Azimio pale Mtongani na nyumba 40 ziliharibika vibaya.

Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kuwatuma wataalam wake kwenda kufanya tathmini na kuwalipa wananchi walioathirika na tukio hilo?

Swali la pili, hivi tunavyozungumza hivi sasa kuna taharuki kubwa imezuka kwa wakazi wanaokaa pembezoni mwa barabara ya Davis Corner - Jet Rumo ambapo wananchi waliokuwa pembezoni mwa barabara hiyo wanawekewa alama za ‘X’ kwamba wavunje nyumba zao ambao kimsingi zimejengwa kihalali kwa sababu wakati wa upanuzi wa barabara walilipwa mita 15 na

Serikali ilikuwa haina pesa ya kuwalipa mita nyingine 15 kukamilisha mita 30 kila upande.

Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa yuko tayari sasa kuamulu zoezi linaloendelea katika Kata ya Vituka, Buza, Makangarawe na Tandika hivi sasa, lisimame mpaka yeye na mimi tutakapokwenda kukaa na wananchi na kujua nini tatizo la pale?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, maswali uliyoyauliza yanahusu masuala ya fidia ambayo inashughulikiwa chini ya sheria maalum chini ya Wizara ya Ardhi. Tumekubaliana kwamba tukutane wote sisi na Wizara ya Ardhi, tulichunguze hilo suala ulilolileta ili hatimaye tukupe majibu sahihi.

**NAIBU SPIKA:** Swali la nyongeza kule nyuma, Mheshimiwa Mtolea si ulishauliza swali au?

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri amejibu swali la pili, la kwanza hajalijibu. Swali la kwanza nilikuwa nauliza…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtolea anasema hivi amejibu kwa pamoja kwa sababu yote mawili yanahitaji kukaa ili muweze kupatia ufumbuzi hilo suala ulilolieleza, kwamba yote mawili yanahitaji kukaa, hakuna ambalo anaweza akalijibu kwa sasa bila hicho kikao. Pale nyuma ujitambulishe tafadhali.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naitwa Mwalimu Marwa Ryoba Chacha ni Mbunge wa Jimbo la Serengeti.

Kwa kuwa tatizo ambalo liko Temeke ni sawasawa na tatizo ambalo liko ndani ya Jimbo la Serengeti. Katika barabara ambayo ni lami ya kutoka Makutano – Butiama - Nata - Tabora B - Loliondo na kadhalika, ilishafanyika upembuzi yakinifu na *evaluation* kwa wananchi ambao barabara hiyo inapita ambapo hiyo barabara haikuwepo. Tangu mwaka 2005 mpaka leo wananchi hao hawajalipwa.

Je, Serikali inasema nini kuhusu fidia ya wananchi ambao wako kando kando mwa hiyo barabara ambao walishafanyiwa *evaluation* lakini hawajalipwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuomba awe na subira kwa sababu kuna swali hilo hilo limeletwa na litajibiwa katika Mkutano huu kabla haujaisha. Kwa hiyo, nitaomba muda ukifika wa kulijibu hilo swali tuyajibu hayo yote kwa pamoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tuendelee, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, Mbunge wa Mwibara aulize swali lake.

Na. 45

**Kuanza kwa Mradi wa *MACEMP* katika Jimbo la Mwibara**

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA** aliuliza:-

Mapambano dhidi ya uvuvi haramu katika Bahari ya Hindi yamekuwa yakihusisha njia ya kuwanyang'anya zana haramu wavuvi wadogo kupitia mradi wa *MACEP* na kuwapatia zana za uvuvi zinazoruhusiwa:-

(a) Je, mradi huo umefanikiwa kwa kiwango gani?

(b) Kama umefanikiwa; je, ni lini mradi huo utaanzishwa kwa wavuvi wadogo wa Jimbo la Mwibara katika Ziwa Victoria?

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kangi Lugola, Mbunge wa Mwibara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa usimamizi wa mazingira ya Ukanda wa Pwani na Bahari *Marine and Coastal Environment Management Project (MACEMP)* ulitekelezwa mwaka 2005/2006 hadi 2012/2013 katika Halmashauri 16 za Ukanda wa Pwani upande wa Tanzania Bara na Halmashauri kumi kwa upande wa Tanzania Zanzibar. Lengo la mradi huu lilikuwa kuimarisha usimamizi na matumizi ya rasilimali za uvuvi katika Bahari Kuu na kuinua hali ya maisha za jamii hizi za Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi wa *MACEMP* umekuwa na mafanikio kadhaa ikiwemo kuimarisha usimamizi wa rasilimali na uvuvi katika Ukanda wa Pwani kwa kuanzisha mamlaka ya usimamizi na uvuvi katika Bahari Kuu yaani (*Deep Fishing Authority)* kuwepo kwa mtambo wa kufuatilia mwenendo wa meli pamoja na kuwezesha kununuliwa kwa boti 16 za doria. Lakini pia kumekuwepo na kuwezesha uendeshaji wa doria katika nchi kavu na anga na kuwezesha kuanzishwa kwa vikundi 182 vya usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi, yaani *Beach Management Units (BMUs)*. Pia vikundi 47 vyenye wavuvi 193 na wavuvi 436 kutoka katika Hifadhi ya Bahari za Mafia na Mtwara walipatiwa zana za uvuvi na kuondokana na matumizi ya zana haramu.

Vilevile mradi umewezesha jamii za Pwani kuibua miradi midogo 470 ya kiuchumi yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 6.6 ambayo ililenga kuboresha

maisha ya Jamii hizo na kunufaisha wananchi wapatao 8000. Aidha, mradi uliwezesha ujenzi wa mialo mitatu ya kisasa ambayo ni pamoja na mwalo wa samaki Kilindoni ulioko Mafia, Masoko ulioko Kilwa na Nyamisati ulioko Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba muda wa kutekeleza mradi wa *MACEMP* umemalizika na Serikali itatekeleza miradi yenye malengo kama hayo katika maeneo mbalimbali ikiwemo Mwibara kutokana na uwezo wa Serikali. Miradi yenye malengo sawa na *MACEMP* imekuwa ikitekelezwa katika Ukanda wa Ziwa Victoria ambayo ni pamoja na Mradi wa Utekelezaji wa Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi katika Ukanda wa Ziwa Victoria uliotekelezwa mwaka 2003 hadi Agosti, 2010 ambao umesaidia ukuaji na uendelezaji wa uchumi katika Ukanda huo na rasilimali za uvuvi zilizoko katika Ziwa Victoria.

Pili, Mradi wa Usimamizi wa Mazingira Ziwa Victoria wa Awamu ya Kwanza na ya Pili na Tatu kumekuwepo na utekelezaji wa pili ambao ulitekelezwa hadi mwaka 2005 na kwenda hadi mwaka 2013 ambao ulikuwa na malengo hayo hayo. Mradi huu umewezesha kuimarika kwa usimamizi wa matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi na kuongeza ajira  na kuboresha huduma za uvuvi katika jamii hizo zinazozunguka Ukanda wa Ziwa Victoria.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa majibu yake na hasa swali langu la (a) amelijibu kikamilifu na kuonyesha ni kwa kiwango gani mradi huu wa *MACEMP* umeweza kuwasaidia wavuvi hasa hawa wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la (b) bado nina wasiwasi kidogo naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa swali langu la msingi lililenga Ziwa Victoria na hususani Mwibara wavuvi na wao wapate mradi huu wa kuwapa nyavu zinazoruhusiwa halafu wanachukua zile nyavu zisizoruhusiwa ili kuwasaidia wavuvi wadogo badala ya kuendelea kuchoma nyavu zao na wakashindwa kupata nyavu zingine ili waweze kujikimu katika maisha yao. Sasa kwa kuwa amesema Serikali itaanzisha miradi kama hii, naomba Mheshimiwa Waziri awahakikishie Wanamwibara kwamba mradi huu utakapoanza Wanamwibara ndiyo watakao kuwa wa kwanza kunufaika na mradi huu wa kuwapatia wavuvi nyavu badala ya kuwachomea nyavu zao?

Swali la pili, kwa kuwa katika majibu yake ameelezea kwamba manufaa mojwapo ya mradi huu ni kuanzisha kwa *BMU* hao walinzi wa rasilimali, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Waziri, *BMU* hizi katika Ziwa Victoria kimekuwa ni kichaka cha kuwasumbua na kuwanyanyasa wavuvi, kimekuwa ni kichaka

cha kuwa-*harass* na kuwasumbua akina Mama kuwanyang'anya samaki, kumwaga samaki katika mwavuli wa *BMU*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na sasa hivi pale Kibara pale kwenye Kijiji cha Mwibara kinamama juzi wamenyang'anywa samaki na matokeo yake…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lugola naomba uulize swali tafadhali.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Ndiyo nauliza. Serikali itatoa kauli gani kwa *BMU* nchi nzima ambao sasa *BMU* wa Kibara pale wanaitwa Boko Haram ambao wamewanyang'anya akina mama samaki na kuwatoza faini ya *cement* mifuko nane na shilingi 5,000/= wakiongozwa na *VEO* Ndugu Moshi, Azimio Lufunjo, Nyafuru Mgoli, Fredy Moma, Kabezi Chitalo, Mrungu….

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lugola unavunja Kanuni sasa.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataja watu ambao wanawanyanyasa akina Mama Serikali inatoa kauli gani?

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa Lugola. Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Lugola alichofanya hakiruhusiwi na Kanuni huruhusiwi kuanza kutaja majina ya watu Kanuni ya 40. Mheshimiwa Waziri naomba ujibu sehemu ya swali ambayo haihusu hiyo ambayo imevunja Kanuni, ahsante.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mafanikio ya mradi huu katika maeneo mbalimbali na nia ama azma ya Serikali ya kutekeleza miradi ya aina hiyo katika maeneo mbalimbali ikiwemo Mwibara, kwa kuwa Mbunge amesema anahitaji niwahakikishie wananchi wake, na mimi niseme kwamba tutakapokuwa tumeshapata uwezo huo nilioutaja na tukaanza kutekeleza kwa kuwa Mbunge ni mdau mkubwa wa kukomesha uvuvi haramu ambao amesema wananchi wake wakipewa zana wataachana na uvuvi haramu, na mimi nimhakikishie kwamba na yeye Jimbo lake na Wilaya yake itakuwa katika maeneo ya vipaumbele vya kuweza kupata mradi huo ili waachane na uvuvi haramu.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumuuliza swali la nyongeza Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *MACEMP* Awamu ya Kwanza, ilipeleka nguvu nyingi sana katika udhibiti kwa maana ya ununuaji wa boti, ujenzi wa majengo kwa ajili ya watumishi na kupeleka nguvu ndogo sana kwa wavuvi. Ukiangalia kilimo ni pamoja na uvuvi, lakini upande wa wakulima wanawezesha pembejeo na elimu.

Je, ni lini wavuvi na wenyewe watawezeshwa kwa kupewa zana bora na elimu badala ya kila siku kuwadhibiti, kuwafukuza na kuwatoza faini kama ambavyo tunafanya?

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze kwa kazi anayoifanya nzuri ya kufuatilia kazi ya wananchi wake ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inajipanga katika hatua za kuboresha sekta ya uvuvi kuwaangalia na wavuvi wenyewe ikiwemo kuanzia shughuli yenyewe ya uvuvi, ikiwemo adha wanayokutana nayo yakiwemo makato, tozo wanazotozwa lakini pia na uhitaji wa vitendea kazi na kuhakikisha pia kwamba tunawaondolea manyanyaso wanayopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitoe kauli tu kwa wale ambao wanawanyanyasa wavuvi, wanawanyanyasa akina mama sambamba na yale ambayo tumetoka kuyasikia, ni vema wakazingatia sheria na misingi ya kazi walizotumwa. Kumekuwepo na utaratibu wa baadhi ya watu wanaopewa dhamana, wakipewa mgambo wanatumia kigezo cha sheria, lakini wakiwapokonya maskini wale kama ni chakula wanakula wao wenyewe, wakipewa kazi ya kuzuia sehemu ya kuuzia nguo wakienda pale kuzuia wanapokonya nguo zile wanachukua wanazitumia wao wenyewe. Hivyo hivyo, na kwenye samaki wanawapoka samaki wanachukua wao wenyewe, tabia hiyo waiache na ikitokea katika eneo lolote tupate taarifa ili sheria iweze kuchukua mkondo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anayenyang'anya wananchi wanaofanya kazi fulani, akawanyang'anya kwa kigezo cha kutumia sheria na akatumia yeye kwa manufaa yake binafsi ni mwizi kama mwizi mwingine anayenyang'anya katika kipindi ambacho wananchi hawaoni. Kwa hiyo, tabia hiyo iachwe na kwa wale watakaoendelea watafikishwa katika mkono wa sheria ili kuweza kukomesha tabia hiyo nchi yetu iweze kuendeshwa kwa misingi ya sheria na utawala bora.

**NAIBU SPIKA:** Tuendelee Waheshimiwa. Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, Mbunge wa Mchinga aulize swali lake.

Na. 46

**Pembejeo Kwa Wakulima wa Ufuta - Lindi**

**MHE. HAMIDU H. BOBALI** aliuliza:-

Wakulima wengi Mkoani Lindi wameamua kujikita katika zao la ufuta ambalo ndilo zao la biashara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima hao kupata pembejeo kupitia Mfuko wa Pembejeo.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamidu Bobali Mbunge wa Mchinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa zao la ufuta ambalo linalimwa kibiashara katika Mikoa ya Kusini yaani Lindi, Mtwara na Ruvuma na maeneo mengine tangu mwaka 1940. Mikoa hiyo huzalisha zaidi ya asilimia 75 ya ufuta wote unaozaishwa hapa nchini. Ufuta, hutumika kama chakula kwa binadamu, na vilevile hutumika kama chakula kwa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la ufuta hustawi zaidi kwenye ardhi yenye rutuba ya asili na kwamba kiasi kidogo cha mbolea ya chumvichumvi, kinahitajika ndiyo maana wakulima hupendelea zaidi kulima kwenye ardhi mpya kwa kila msimu. Hata hivyo, ili kupata mavuno mengi, inahitaji kiasi kidogo cha mbolea za kupandia na kukuzia, na hivyo kulingana na hali ya udongo katika eneo husika kunahitajika mbolea .

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mpango wake wa ruzuku kwa wakulima inaangalia uwezekano wa kuongeza mazao mengine ikiwemo ufuta pale bajeti itakaporuhusu. Hata hivyo, kwa kuwa wakulima wa Mkoa wa Lindi wameamua kulima ufuta kama zao lao la bishara, Serikali inawashauri Wakulima wa Mkoa wa Lindi kupitia kwenye vikundi vyao vya ushirika kuomba mikopo kwenye Mfuko wa Taifa wa Pembejeo ili kuweza kujihakikishia upatikanaji wa pembejeo na kwa namna ya soko huria.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuulize swali moja la nyongeza Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, tatizo la pembejeo lililopo kwenye zao la ufuta lipo pia kwenye zao la korosho ambalo ni zao la pili la biashara Mkoa wa Lindi. Changamoto ya pembejeo Mkoa wa Lindi inatokana na

utofauti wa maeneo na hali ya hewa. Pembejeo inayoletwa Lindi, Sulpha inaletwa mwezi wa 5 mwezi wa 6 ambao kwa Mchinga wakati huo inakuwa tayari korosho zimeishaanza kuzaa, lakini maeneo mengine ya Tandahimba na Masasi yanakuwa bado.

Je, Serikali ipo tayari sasa, kusambaza pembejeo ya zao la korosho ifikapo mwezi wa tatu ili korosho zinazowahi katika Jimbo la Mchinga ziwahi kupuliziwa na hizo pembejeo.

**WAZIRI WA KILIMO MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru sana kwa swali lake la nyongeza ni swali zuri ambalo linahusisha pia pembejeo zinazotolewa kwa mazao mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba Wizara yangu, inapanga kuangalia, utaratibu mzima wa utoaji ruzuku, kama nilivyosema jana. Lakini katika kuangalia kwake, nimewaagiza wataamu wangu kila mtaalamu anayesimamia ugawaji wa pembejeo ama mbegu katika eneo husika awe na bango kitita linaloonesha msimu unaanza lini katika eneo gani, na kuhakikisha kwamba Serikali tunasimamia upatikanaji wa ruzuku ama pembejeo husika, kama ni mbegu angalau mwezi mmoja kabla ya msimu kuanza ili kuweza kuwapa fursa wakulima kupata pembejeo hizo kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliongea na wataalam wangu ni aibu kwa watu waliosoma wakaaminiwa na Serikali, wakaaminiwa na wananchi wakapewa dhamana kupeleka mbegu ama mbolea ya kupandia, wakati eneo husika watu wako kwenye kupalilia na walishapanda mbegu zao na walishatumia mbolea yao. Kwa hiyo, nimeagiza watu wawe na bango kitita ambalo itasaidia kuwa na uelewa na kuwa na kitu cha kuangalia tunapopeleka pembejeo, tupeleke kwa wakati angalau mwezi mmoja kabla ya msimu kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaombe Wabunge, katika maeneo yenu nifikishieni kila mmoja kutoka kwake na mimi nitakuwa na bango kitita langu, anapendekeza mbegu ama pembejeo iwe imeishafika katika eneo lake ifikapo muda gani, na hiyo ndiyo nitakayotumia kusimamia Wizarani kwangu. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, kwa sababu hapa Tanzania tunayo mazao makuu ya biashara, ambayo yalikuwa yanajulikana katika kuongeza uchumi wa nchi yetu ambayo ni pamba, kahawa, korosho pamoja na katani.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba mazao haya ambayo yalikuwa yanatoa ajira kubwa, uchumi kwa nchi yetu, kwamba mazao haya sasa yanatafutiwa soko lenye uhakika hasa pamba ambayo zaidi ya Mikoa 14,

Wilaya 42 zilikuwa zinategemea zao la pamba, Serikali ina mpango gani hasa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Ndassa, Mbunge wa Sumve kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana kwa kazi yake nzuri ya Ubunge aliyoifanya na Wabunge wengi wapya tuige kwake, maana yake Mheshimiwa Ndassa ameaminiwa na wananchi wake kwa muda mrefu kwa ajili ya kufanya kazi nzuri namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango mzuri sana wa kuendeleza mazao yote ya biashara, mpango wa kwanza ambao Serikali imeweka uzito mkubwa ni kuanzia kwenye ubora wa zao, kwa sababu ubora wa zao una uhusiano wa moja kwa moja na upatikanaji soko lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili ambalo Serikali imeweka mkazo mtasikia hata kwenye Mpango utakapowasilishwa na Dkt. Mpango muda siyo mrefu, imeweka mkazo kwenye kuongeza thamani ya mazao, kwa sababu na yenyewe ni hatua nzuri unapoenda kwenye kupata soko la zao husika na baada ya hapo tukishaongeza thamani kwa kupitia viwanda tutakuwa na uhakika wa kuweza kuuza mazao yanayotokana na mazao yetu ya biashara kwa bei ambayo itawaletea manufaa wanachi wetu na kuweza kuwafanikisha kuweza kuchochea watu wengi kujihusisha na uzalishaji wa mazao hayo kwa sababu yatakuwa na tija.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2014 zao la korosho lilivunja rekodi ya uzalishaji mpaka tani laki mbili kwa mwaka, lakini zao la pamba lilishuka uzalishaji wake kwa takribani asilimia 40, na bado nchi yetu inauza korosho nje kama korosho ghafi, ilihali kulikuwa na viwanda vingi ambavyo vilijengwa na Baba wa Taifa takribani viwanda 12, na baadhi ya viwanda sasa hivi vimegeuka kuwa ni ma-*godown* kwa ajili ya stakabadhi ghalani.

Serikali inachukua hatua gani ya kuhakikisha kwamba korosho zote ambazo zinazalishwa nchini zinabanguliwa kwanza hapahapa nchini kabla ya kupelekwa nje na kutungeneza ajira nje? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba nitoe jibu kwa Mheshimiwa Zitto, Mbunge wa Kigoma Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda vya korosho vilivyobinafsishwa na kugeuzwa maghala, *Treasury Registrar* ametoa malekezo na wito wote wajisalimishe kwao waeleze kwa nini wamekiuka misingi ya mauziano. Misingi ya mauziano ilikuwa ni kwamba walipe pesa kidogo kusudi viwanda vile waendelee kuvitumia kwa kubangua korosho na kutoa ajira. Kwa hiyo, tangazo limetolewa na muda wake umeishakwisha kwa hiyo asiyeenda anakiuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ubanguaji wa korosho. Ubanguaji wa korosho ndiyo msimamo wetu na wiki iliyopita niliongea na Balozi wa India anasema wao hawana matatizo. India wamefungua dirisha kwa mazao ya Tanzania yapatayo 480 anasema hana tatizo, na taarifa yako Mheshimiwa Zito na watu wa Kanda ya Korosho, kuna kampuni imeishaanza mchakato wa kujenga viwanda vipya katika ukanda wa korosho na wanasema korosho yote iliyopo haitoshelezi viwanda vyao wakianza kazi, na wameniomba niwape hata kibali cha kuagiza korosho nyingine kutoka nje ya nchi nimesema hapana, wasaidieni wananchi wetu kulima zaidi ili mbangue na muuze huko duniani.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 43 muda wetu wa maswali umekwisha, sasa nitasoma matangazo kadhaa niliyonayo.

Tangazo la Mkutano, Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake anaomba Wabunge Wanawake wote Kukutana katika Ukumbi wa Msekwa saa 7 mchana leo. Tarehe 29/01/2016, tangazo limetolewa na Makamu Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Chenge Mwenyekiti atakuja kunipokea sasa kuendelea na Hoja za Serikali. Mheshimiwa Chenge.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alikalia Kiti*

**NDG. RAMADHAN I. ABDALLAH - KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali kwamba Bunge sasa lijadili na kuidhinisha Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kwa kipindi cha miaka mitano kinachoanzia 2016/2017 hadi 2020/2021 *(The Framework of the Second five years Development Plan 2016/2017 - 2020/2021*).

## HOJA ZA SERIKALI

### Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kwa kipindi cha miaka mitano kinachoanzia 2016/2017 hadi 2020/2021*(The Framework of the Second five years Development Plan 2016/2017 - 2020/2021*)

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Mtoa Hoja.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo!

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja..

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Naomba Mwongozo wako Mheshimiwa Mwenyekiti. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7) kwa sababu ya muda naomba nisiisome.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nakusihi keti kitako, tunaendelea na hoja iliyo mbele yetu.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mwongozo Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Nimemuita Mtoa Hoja kwa shughuli iliyo mbele yetu.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Siongelei *issue* ya *TBC* naomba mwongozo Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Nitachukua Miongozo yenu mwishoni huko tutakapotaka kusimamisha shughuli za leo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, lipokee na kujadili mapendekezo, ya mwelekeo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa miaka mitano 2016/2017 mpaka mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kutuwezesha kushiriki Mkutano wa Pili wa Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kipekee napenda kutumia fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Makamu wa Rais, kwa kuchaguliwa kwao kuingoza nchi yetu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waheshimiwa Mawaziri wote kwa kuteuliwa kushika nafasi hizo muhimu katika uongozi wa nchi yetu.

Pia ninampongeza Mheshimiwa Job Yustino Ndugai Spika na Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwao kuongoza Bunge letu Tukufu. Aidha, ninakupongeza wewe Mwenyekiti na Wenyeviti wenzako ambao mmechaguliwa kumsaidia Mheshimiwa Spika. Lakini pia nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kwao kuwawakilisha wananchi katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine ninapenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa aliyonayo kwangu kuniteua kuwa Waziri wa Fedha na Mipango. Ninaahidi kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa kwa umakini na uhaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru kwa dhati kabisa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo kwa ushirikiano wao. Maelekezo na ushauri mzuri waliotupatia wakati wa kujadili Mapendekezo ya Mwelekeo wa Mpango wa Pili wa Maendeo wa miaka mitano umetusaidia katika kuandaa hotuba hii na kuboresha hatua za maandalizi ya mango wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninamshukuru Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Servacius Beda Likwelile, kwa ushirikiano walionipa katika, kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiaw Mwenyekiti, mapendekezo ya mwelekeo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa miaka mitano 2016/2017 na 2020/2021 ninayowasilisha leo ni kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara ya 63(3)(c), ambayo inalitaka Bunge kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya mwelekeo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa miaka mitano, yameandaliwa kwa kuzingatia Mpango elekezi wa Miaka 15. Kuanzia mwaka 2011/2012 mpaka 2025/2026 wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango elekezi ulitokana na mapitio yaliyofanyika katika mwaka 2010 kwa miaka kumi ya utekelezaji wa dira ya mwanzo. Katika mapitio hayo, ilionekana wazi kuwa ipo haja ya kujipanga upya kutuwezesha kufikia malengo ya dira ndani ya kipindi cha miaka 15 ililyokuwa imesalia. Hivyo ilipangwa kuwa utekelezaji uwe katika awamu tatu za Mipango ya Maendeleo ya miaka mitano mitano na kila Mpango uwe na dhima maalum kuendana na muelekeo wa mpango wenyewe.

Mhehimiwa Mwenyekiti, aidha, ilipendekezwa kuwa Mpango wa miaka mitano utatekelezwa kupitia Mpango wa mwaka mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa miaka mitano 2011/2012 mpaka 2015/2016 unafikia ukomo wake mwezi Juni, 2016.

Dhima ya Mpango huo ilijielekeza katika kutanzua vikwazo vya ukuaji wa uchumi na kubainisha maeneo ya kipaumbele kuwa ni miundombinu, kilimo, viwanda, maendeleo ya rasilimali watu, huduma za fedha, utalii na biashara. Ili kuendeleza utekelezaji wa mpango elekezi, Serikali sasa inawajibika kuandaa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa miaka mitano utakaokuwa mwongozo wa kuandaa mipango na Bajeti ya kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano ijayo kuanzia mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia Mpango elekezi, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa miaka mitano ulipaswa kujikita katika kujenga misingi ya uchumi wa viwanda. Hata hivyo, mwaka 2015 Serikali ilifanya uamuzi wa makusudi kuunganisha Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano na MKUKUTA ili kujumuisha ajenda ya kupunguza umaskini, na Mipango ya Maendeleo ya Taifa. Msingi wa uwamuzi huo ni kuwa na mfumo mmoja wa utekelezaji wa Mipango, na hivyo kutanzua changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mipango pacha. Miongoni mwa changamoto hizo ni kuwepo kwa vipaumbele vinavyofanana na hivyo kugawanya rasilimali za Taifa katika utekelezaji na kuwepo kwa mfumo dhaifu katika kuratibu na kutathmini utekelezaji wa mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo uamuzi wa kuunganisha Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano na MKUKUTA unatarajiwa kujumuisha msukumo wa kupunguza umaskini katika mipango ya maendeleo ya Taifa na kuimarisha uratibu, ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa vipaumbele vya mpango. Kufuatia uamuzi huo Mpango wa Pili wa Maendeleo wa miaka mitano utahusisha kwa pamoja masuala ya maendeleo ya viwanda na maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekeo ya mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano umezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 hususan msukumo wa kujenga uchumi wa viwanda na kuongeza kasi ya kupunguza umaskini. Vilevile mapendekezo haya yamezingatia maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyoyatoa wakati akifungua Bunge la Kumi na Moja. Makubaliano ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeyaridhia ikiwa ni pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030, Dira ya Afrika ya Mwaka 2063, Mpangokazi wa Kuharakisha Maendeleo ya Viwanda Afrika ya mwaka 2008, Sera ya Viwanda ya Afrika Mashariki pamoja na Mkakati wa Utekelezaji wake. Lakini pia Mwelekeo wa Maendeleo ya Viwanda wa SADC wa mwaka 2016 – 2018, na Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda wa *SADC* wa mwaka 2015 – 2063.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nianze kuelezea mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa miaka mitano lakini pia MKUKUTA Namba Mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mwenendo wa uchumi. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa miaka mitano na MKUKUTA II, uchumi nchini umekua kwa wastani wa asilimia 6.7, ukuaji huo ulichangiwa na sekta ya madini na gesi, ujenzi, uzalishaji na mauzo ya nje ya bidhaa za viwandani na huduma za fedha. Hii ilichangiwa pia na kuwepo kwa hali nzuri ya hewa na amani na utulivu nchini. Hata hivyo, ukuaji huu ni mdogo ikilinganishwa na lengo la kufikia wastani wa asilimia nane kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia ukuaji huu pato la kila mtu limeongezeka kutoka wastani wa shilingi 770,464 sawa na dola za Kimarekani 537.9 mwaka 2010, kufikia shilingi 1,724,415 ambazo ni sawa na dola 1,043 mwaka 2014. Kiwango hiki bado ni chini ya lengo la Dira ya Taifa ya Maendeleo la dola 3,000 ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa miaka mitano mfumuko wa bei ulipungua kutoka wastani wa asilimia 12.7 mwaka 2011 kufikia asilimia 5.6 mwaka 2015. Viwango vya riba vinaonesha kuendelea kuimarika ambapo tofauti kati ya riba za amana na mikopo ya mwaka mmoja ilipungua kutoka asilimia 4.59 Disemba 2011 hadi asilimia 3.22 Oktoba 2015. Thamani ya mauzo nje ya bidhaa na huduma iliongezeka kutoka dola za Kimarekani milioni elfu saba mia tatu tisini na nane mwaka 2011 hadi dola milioni elfu tisa mia nne na sita nukta moja Oktoba 2015, sawa na ongezeko la asilimia 21.3

Pamoja na mafanikio hayo, mfumo wa uzalishaji na mauzo nje bado unategemea kwa kiasi kikubwa mazao ghafi. Hivyo Serikali inaelekeza nguvu zake kuweka misingi ya kusukuma maendeleo ya viwanda ili kubadili hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya shilingi. Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Kimarekani iliendelea kupungua kutoka wastani wa shilingi 1,566.7 Disemba 2011 hadi shilingi 2,177.1 Oktoba 2015. Hali hii inaashiria kuwa mahitaji ya fedha za kigeni katika kuendesha uchumi nchini ni makubwa kuliko kiasi cha fedha kinachopatikana kutokana na mauzo nje ya nchi. Hivyo, ipo haja ya msingi ya kuongeza mauzo nje ya bidhaa na huduma ili kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Miaka Mitano unakadiriwa tutakapofika Juni 2016 utakuwa umefikia kati ya asilimia 50 na 60 ya malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya ufanisi wa utekelezaji wa baadhi ya maeneo ya kipaumbele ya Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano na MKUKUTA Namba Mbili ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza miundombinu, na nianze na miundombinu ya nishati. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa nishati ya umeme kufikia *megawatt* 1,246.24 mwaka 2014 kutoka *megawatt* 900 mwaka 2010. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 44.8 ya lengo la kufikia *megawatt* 2,780 mwaka 2015. Ni matarajio ya Serikali kuwa kasi ya uzalishaji wa nishati ya umeme itaongezeka kufuatia kukamilika kwa ujenzi wa bomba la kusafirishia gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam, lakini pia Kiwanda cha kuchakata gesi cha Madimba na vituo vya kupokea gesi vya Somangafungu na Kinyerezi na mtambo wa kufua umeme wa Kinyerezi I.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa barabara na reli. Serikali imekamilisha ujenzi na ukarabati wa barabara za lami zenye urefu wa kilometa 2,775, sawa na asilimia 53.3 ya lengo la kujenga kilometa 5,204. Aidha, imekamilisha ukarabati wa kilometa 150 za reli katika kiwango cha ratili 80 kwa yadi, sawa na asilimia 76.1 ya lengo la kilometa 197 ifikapo Juni 2016.

Pia ununuzi wa vichwa vya treni na mabehewa ya abiria, mizigo na ya *brake* umewezesha kuanza kwa safari za treni katika reli ya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa usafiri wa anga. Kwa upande wa viwanja vya ndege Serikali imekamilisha ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Songwe na ukarabati wa viwanja vya Arusha, Bukoba, Kigoma, Mafia, Mpanda na Tabora. Hii imesaidia kuongeza idadi ya abiria waliotumia usafiri wa anga kutoka 3,437,608 mwaka 2011 hadi 5,059,739 mwaka 2014 likiwa ni ongezeko la asilimia 47.2

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bandari kumekuwa na ongezeko la uwezo wa kuhudumia mizigo bandarini kutoka tani 7,130,000 mwaka 2011/2012 hadi tani 14,600,000 mwaka 2014/2015 sawa na ongezeko la asilimia 104 dhidi ya lengo la tani 9,870,000. Ongezeko hili lilitokana na kuongezwa kwa muda wa huduma bandarini na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya upakiaji na upakuaji wa shehena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa TEHAMA, ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa wenye urefu wa kilometa 7,560 ulikamilishwa na kusambazwa katika mikoa 24 ya Tanzania Bara na Zanzibar ikiwa ni asilimia 100 ya malengo. Aidha, Mkongo huo umeunganishwa na nchi jirani za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Zambia na Malawi. Hali hii inaipa Tanzania fursa ya kipekee kupanua matumizi ya TEHAMA nchini na kuendesha biashara ya huduma hiyo na nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa kilimo. Uzalishaji katika sekta ya kilimo uliongezeka kutoka wastani wa asilimia 2.7 kabla ya mwaka 2010 kufikia wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2010 na 2014. Ongezeko hili bado halikufikia lengo la asilimia sita kwa mwaka. Hata hivyo, tija kwa baadhi ya mazao kama vile mahindi, mpunga na miwa imeongezeka kwa kiasi kikubwa. Aidha, eneo la kilimo cha umwagiliaji limeongezeka kutoka hekta 345,690 mwaka 2010/2011 na kufikia hekta 461,326 mwaka 2014/2015, sawa na asilimia 46 ya lengo la hekta 1,000,000 ifikapo Juni, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa viwanda. Mchango wa sekta ya viwanda katika fedha za kigeni uliongezeka kutoka asilimia 17 mwaka 2012 hadi asilimia 23 mwaka 2014 ya mapato ya mauzo nje, ikiwa ni zaidi ya lengo la kufikia asilimia 19.1 mwaka 2015. Aidha, kiwango cha ajira kwa sekta ya viwanda kiliongezeka kutoka asilimia 2.6 mwaka 2012 kufikia asilimia 3.1 mwaka 2014 ya ajira nchini. Vilevile mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia saba ikilinganishwa na lengo la kufikia asilimia 12.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mazingira wezeshi kibiashara Tanzania ilishika nafasi ya 126 mwaka 2010, nafasi ya 134 mwaka 2014 na nafasi ya 140 mwaka 2015, na inatarajiwa kushika nafasi ya 139 mwaka huu wa 2016 kati ya nchi 186 katika mazingira ya uendeshaji biashara kwa vigezo vya Benki ya Dunia. Kigezo hiki ni muhimu katika kubainisha uwezo wa nchi kushindana kibiashara na kuvutia uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hali hii juhudi zilizochukuliwa hivi karibuni zimeanza kuonesha mafanikio ya kuridhisha, hususan kuimarika kwa upatikanaji wa umeme na miundombinu ya barabara mijini na vijijini. Aidha, huduma ya utoaji vibali vya ujenzi imeimarika. Tuna uhakika kuwa matokeo ya juhudi hizi na nyingine za maboresho zinazoendelea nchini zitapandisha nafasi ya Tanzania katika kipindi kifupi kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nieleze kidogo kuhusu maendeleo ya watu na huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza elimu na kwa upande wa vyuo vya elimu ya juu, udahili uliongezeka kutoka wanafunzi 262,376 mwaka 2010/2011 hadi wanafunzi 362,880 mwaka 2013/2014. Hali inatarajiwa kuimarika zaidi mara ujenzi wa *campus* ya Mloganzila ya Chuo Kikuu cha Tiba Muhimbili na ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma utakapokamilika.

Aidha, wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo vya ufundi waliongezeka kutoka 104,840 mwaka 2011 hadi 164,077 mwaka 2014 ikiwa ni chini ya lengo la wanafunzi 166,132 ifikapo mwisho wa mwaka 2015. Kwa upande wa elimu ya

msingi na Sekondari kumekuwa na mafanikio ambapo idadi ya wanafunzi wanaokatisha masomo kwa ngazi ya elimu ya msingi ilipungua kutoka 68,015 mwaka 2012 hadi 67,087 mwaka 2014 na kwa upande wa sekondari ilipungua kutoka 94,990 mwaka 2012 hadi 80,153 mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa afya. Upatikanaji wa huduma za afya umeimarika japokuwa ni chini ya malengo. Idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano vilipungua kutoka 81 mwaka 2010 hadi vifo 54 mwaka 2013 ikilinganishwa na lengo la vifo visivyozidi 45 kwa kila watoto 1,000 wanaozaliwa hai. Vifo vya mama wajawazito wakati wa kujifungua pia vimepungua kutoka 454 mwaka 2010 na takribani vifo 432 mwaka 2013 kwa kila vizazi 100,000 ambapo lengo lilikuwa kufikia vifo visivyozidi 175 mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania pia imefanikiwa kupunguza viwango vya maambukizi mapya ya magonjwa makubwa kama vile UKIMWI, malaria, kifua kikuu na ukoma. Kwa ujumla Tanzania imevuka nusu ya malengo ya milenia katika eneo hili.

Aidha, kiwango cha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa maeneo ya vijijini kiliongezeka kutoka asilimia 57.8 mwaka 2010/2011 kufikia asilimia 68.8 mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa huduma za fedha biashara na utalii, Serikali iliweka lengo la kuimarisha mtaji wa Benki ya Rasilimali *(TIB)* na kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo *TADB* kwa kuwekeza kila mwaka kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa kila Benki. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2014 mtaji wa *TIB* umefikia shilingi bilioni 212, na *TADB* ilizinduliwa ikiwa na mtaji wa shilingi bilioni 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa biashara; mauzo ya Tanzania duniani yalipanda kidogo kutoka asilimia 0.04 ya mauzo yote duniani yaani *global export* mwaka 2010 kufikia 0.048 mwaka 2014. Hata hivyo, ongezeko hilo ni chini ya lengo la kufikia asilimia 0.1 ifikapo mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utalii; wageni wa nje walioitembelea Tanzania waliongezeka kutoka 784,709 mwaka 2010 hadi 1,142,217 mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 46, na kuvuka lengo la ongezeko la asilimia 40 ifikapo mwisho wa mwaka 2015. Aidha, mapato katika Sekta ya Utalii yaliongezeka kutoka dola za kimarekani milioni 1,254.5 mwaka 2010 hadi dola milioni 2006.32. sawa na ongezeko la asilimia 62.5 ikilinganishwa na lengo la asilimia 100 ifikapo Juni, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kupunguza umaskini wa kipato; tafiti za mapato na matumizi katika kaya zinaonesha kuwa kiwango cha umasikini mijini na vijijini kimepungua, hali hiyo inaashiria kuwa ukuaji wa uchumi umeanza kunufaisha wananchi wengi zaidi, umaskini ulipungua kutoka asilimia 39 mwaka 1992, kufikia asilimia 34.4 mwaka 2007 sawa na kupungua kwa asilimia 4.6 kwa kipindi cha miaka kumi na tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umaskini katika kipindi cha miaka mitano ya karibuni ulipungua kwa asilimia 6.2 kutoka asilimia 34.4 mwaka 2007, hadi asilimia 28.2 mwaka 2012. Japokuwa hakuna utafiti uliofanyika hivi karibuni juu ya hali hii, dalili zipo wazi kuwa kuna mabadiliko chanya ingawa yanatofautina kati ya maeneo ya mijini na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla kaya zinazoishi katika nyumba zilizoezekwa na bati, kujengwa kwa matofali ya saruji au ya kuchoma na kumiliki mali za kudumu kama vile pikipiki na baiskeli zinazidi kuongezeka kuashiria kuimarika kwa ubora wa maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utawala bora na uwajibikaji; Tanzania imeendelea kuwa moja ya nchi chache barani Afrika zenye utulivu wa kijamii na kisiasa. Hii ni kielelezo kuwa kuna utawala thabiti, hata hivyo katika miaka ya karibuni hali imeanza kubadilika kidogo. Kumekuwa na ongezeko la matukio yanayoashiria kupungua kwa uvumilivu staha na uzingativu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi na vikongwe japo yamepungua yamechafua sifa nzuri ya nchi yetu. Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea na juhudi za kujenga uwezo wa utoaji huduma na usimamizi wa sheria na utoaji haki, mapambano dhidi ya rushwa na uwajibikaji katika matumizi ya fedha na mali za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mchango wa sekta binafsi. Uwekezaji wa sekta binafsi katika utekelezaji wa mipango, wa mpango umezidi kuimarika mwaka hadi mwaka. Miradi iliyosajiliwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania kati ya mwaka 2011 hadi 2015 ilifikia elfu tatu mia nne thelathini na saba yenye makadirio ya mtaji wa dola za kimarekani milioni 122,207.

Kwa ujumla kumekuwa na ongezeko la mitaji ya uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje, kutoka dola za kimarekani milioni 1813 mwaka 2010 kufikia milioni 2142 mwaka 2014. Ongezeko hili lilichangia kuongezeka kwa mtaji wa sekta binafsi kutoka shilingi bilioni 7570.2 mwaka 2010, hadi bilioni 12861.1 mwaka 2013. Ikidhihirishwa na miradi mikubwa ya viwanda vya saruji na vifaa vya ujenzi, nyuzi na nguo na bidhaa za chakula. Aidha, uhaulishaji wa fedha binafsi kutoka nje uliongezeka kutoka asilimia 0.13 hadi asilimia 0.22 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za utekelezaji. Hizi zilikuwa pamoja na zifuatazo:-

(1) Ni upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

(2) Taratibu ndefu na gharama kubwa za ununuzi wa umma.

(3) Madeni hususani ya wakandarasi wa ujenzi wa barabara.

(4) Urasimu wa upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji.

(5) Upatikanaji wa fedha za kulipa fidia na mapungufu katika taarifa za tathmini ya fidia.

(6) Bajeti ya maendeleo kutegemea kwa kiwango kikubwa misaada na mikopo kutoka nje.

(7) Mchango mdogo wa sekta binafsi kutaka kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

(8) Mazingira yasiyo wezeshi kwa uwekezaji na uendelezaji biashara.

(9) Uhaba wa miundombinu wezeshi.

(10) Uwezo mdogo wa taasisi za fedha hapa nchini kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya miaka mitano na MKUKUTA II ambao utasaidia katika maandalizi ya Mpango ujao, na hatimae utekelezaji, ilikuwa ni pamoja na yafuatayo:-

i. Upatikanaji wa rasilimali, fedha, watu na muda kwa kadri ya mahitaji ya mipango kazi ya utekelezaji, ni vema ukapewa msukumo unaostahili ikiwa ni pamoja na kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuangalia upya utaratibu wa *cash budget* katika kugharamia miradi ya maendeleo.

ii. Ni hatua za makusudi ambazo hazina budi kuchukuliwa ili kuipa nafasi sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi kwa kupitia uwekezaji wa moja kwa moja na kwa njia ya ubia na sekta ya umma.

iii. Ushirikishwaji mpana wa jamii katika hatua zote za mpango, ni muhimu ukapewa msukumo wa kutosha kwani unasaidia kupata muafaka juu ya

vipaumbele vya mpango mgawanyo wa rasilimali, vigezo vya kupima ufanisi wa utekelezaji na mchango wa wadau.

iv. Ni fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kielelezo na Matokeo Makubwa Sasa, hizi ni muhimu zikajalindwa.

v. Hatua za kujenga mazingira wezeshi ya kibiashara zinapaswa kuwa endelevu na ni muhimu zikapewa kipaumbele katika mpango ujao na kwa ajili hii, maboresho na mazingira wezeshi kwa miradi mikubwa ya kipaumbele hayanabudi kubainishwa kwa kutumia utaratibu wa kimaabara unaotumiwa katika miradi ya Matokeo Makubwa Sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikishwaji wa wadau, maandalizi ya mapendekezo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo ambao nitaanza kuyaeleza sasa. Pamoja na matokeo ya mapitio ya utekelezaji wa Mpango na MKUKUTA yamezingatia maoni ya wadau mbalimbali na baadhi ya wadau walioshiriki kutoa maoni ni pamoja na Wizara, Idara na Taasisi za Umma.

**MWENYEKITI:** Hitimisha Mheshimiwa Waziri hoja yako sasa.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti. Napewa dakika ngapi? *One minute!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mapendekezo tunayowasilisha mbele ya meza yako yalijadiliwa katika semina maalum na Wabunge naomba sasa nihitimishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa kunisikiliza aidha hotuba hii na Kitabu cha Mapendekezo ya Mwelekeo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya miaka mitano, vinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango na Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu lijadili mapendekezo niliyoyawasilisha na kufanya maamuzi ili Serikali iendelee na maandalizi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo ya miaka mitano 2016/2017 mpaka mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa wasilisho lako. (*Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu utaratibu wetu ni dakika thelathini kwa Mheshimiwa mtoa hoja. Mwenyekiti nae muda huo huo na Msemaji wa Kambi ya Upinzani dakika 30. Nichukue muda huu pia kutoa matangazo machache ya kazi pamoja na wageni tulio nao hapa.

Nianze na wageni walioko kwenye jukwaa la Spika, tunao wageni saba wa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango, ambao ni Watendaji Wakuu, nadhani wako huku sasa hivi. Watendaji Wakuu kutoka Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Tume ya Mipango karibuni sana. Lakini pia tuna wageni kumi kutoka *UN Women Enhance Cedeo Foundations* wakiongozwa na Bi. Anna Colins, sijui wako wapi nadhani wametoka.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na wageni walioko katika jukwaaa la wageni, tuna wageni sabini na mbili wa Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Kilimo na Uvuvi ambao ni Walimu wawili pamoja na Wanafunzi sabini kutoka Shule ya Sekondari ya Sangu iliyoko Mbeya Mjini, wako wapi wageni wetu kutoka Sangu? Karibuni sana. Someni vizuri kwa faida ya Taifa letu. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Charles Kitwanga, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni wanafunzi wanne kutoka Jimbo la Misungwi ambao wanasoma katika Chuo Kikuu cha St. John's Dodoma. Mko wapi wageni kutoka Misungwi labda wametoka lakini kokote mlipo karibuni sana.

Tuna wageni arobaini na nne wa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda, wanachama 29 wa CCM kutoka Jimbo hilo Mkoani Mara na viongozi 15 wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo cha Mipango kilichopo Dodoma, karibuni sana viongozi na wanafunzi wetu.

Tunao wageni 20 wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, ambao ni viongozi wa wafanyabiashara ndogondogo kutoka Dodoma. Wako wapi karibuni sana.

Pia tuna Wanafunzi watatu kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaosoma mwaka wa tatu ni wageni wa Waziri huyo huyo, wako wapi karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wengine kutoka asasi inayojishughulisha na masuala ya vijana (V*ision for Youth)* ambao ni kama wafuatao, Viongozi sita wa chama hicho pamoja na walimu wawili na wanafunzi arobaini na wawili kutoka shule

ya msingi St. Monica iliyopo Arusha mko wapi, karibuni sana. Pia wageni 42 wa Mheshimiwa Seif Gulamali wa Jimbo la Manonga Mkoani Tabora ambao ni walimu wawili, makocha wawili na wanafunzi 37 wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji *(NIT)* karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunae mgeni wa Mheshimiwa Atashasta Nditiye, Mbunge wa Muhambwe ambaye ni Sina Martin Akilimali, yuko wapi mgeni wetu ametoka haya karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa upande wangu wageni ndiyo walikuwa hao, hii ndiyo orodha niliokabidhiwa kwa hiyo mtaniwia radhi kama yako mengine.

Waheshimiwa Wabunge, lakini kuna matangazo ya kazi. Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI leo saa saba kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo na kitafanyika katika Ukumbi ulioko Jengo la Ofisi la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hapa Dodoma. Sasa mkutane mtaelekezwa pale lilipo jengo hilo saa saba mchana leo.

Waheshimiwa Wabunge, utaratibu wa kupatikana hati za kusafiria za kidiplomasia kwa Waheshimiwa Wabunge na hili ni muhimu limekuwa linaulizwa ulizwa. Ofisi ya Katibu wa Bunge sasa inalitolea taarifa. Mnajulishwa kwamba Ofisi ya Katibu wa Bunge kwa kushirikiana na Idara ya Uhamiaji imeandaa zoezi maalum la kuwapatia Wabunge wote hati za kusafiria za kiplomasia *(Diplomatic Passport)*. Zoezi hili litafanyika kwa muda wa siku nne na litaanza leo Ijumaa Tarehe 29 Januari saa saba mchana hadi saa moja usiku na tarehe 30 Januari na kuendelea hadi tarehe mbili asubuhi. Litaanza saa mbili asubuhi hadi saa moja jioni Ukumbi wa Msekwa.

Zoezi hili litawahusu Waheshimiwa Wabunge wote wasio na hati hizo pamoja na wale ambao hati zao za kidiplomasia zimebakiza miezi sita kumaliza muda wake. Kwa hiyo, angalia *passport* yako kwa wale ambao tayari mnazo, uone muda wako uliobaki uchukue fursa hii kuweza kuingizwa katika mfumo wa kupata *pass* nyingine.

Aidha, vitu vinavyohitajika kuwezesha kupewa hati hizo mtaelezwa mnapoenda kuchukua fomu na zoezi hili ni la kisheria mngesoma sheria husika mtayaona yote hayo mnahimizwa muitumie vizuri fursa hii, wale ambao mko hapa kwenye Bunge hili.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa muda wa *Bunge Sports Club* Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigangwalla anaomba niwajulishe Waheshimiwa Wabunge kuwa kutakuwa na mashindano ya riadha tarehe 30 Januari, 2016 yaani kesho yenye kauli mbiu hapa kazi tu 2016 hapa

Dodoma *half marathon* kilometa tano na kilomita mbili yatakayofanyika mjini Dodoma.

Mashindano hayo yatahusisha jinsia zote, kwa mita 100, mita 200, mita 800 na mita 1500. Hivyo Waheshimiwa Wabunge wote wenye nia ya kushiriki mbio hizo mnaombwa mjiandikishe pale mapokezi kwenye lango kuu ili majina hayo yawasilishwe kwa Chama cha Riadha Mkoa wa Dodoma.

Tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti huyo huyo, anaomba niwajulishe Wabunge kwamba kesho siku ya Jumamosi kwenye Uwanja wa Jamhuri hapa Mjini Dodoma kuanzia saa kumi jioni kutakuwa na mchezo wa mpira wa miguu kati ya Waheshimiwa Wabunge na Benki ya *CRDB* na mechi ya *netball* kati ya Waheshimiwa Wabunge na Chuo cha Usafirishaji *(NIT)*.

Aidha, kocha mkuu wa *Bunge Sports Club* Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu, kwa mara ya kwanza anaweka hadharani kikosi chake cha wachezaji wapya wa Bunge hili la Kumi na Moja, wote mnaombwa kujitokeza kuishangilia timu yetu ya Bunge, tangazo muhimu sana hilo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yapo matangazo mengi lakini muda, pia Jumapili kesho kutwa kutakuwa na mchezo mwingine wa kirafiki wa mpira wa miguu kati ya timu ya *Bunge Sports Club* na timu ya Shirikisho la Vyuo Vikuu, mchezo huo utafanyika saa tatu asubuhi kwenye kiwanja cha Jamhuri. hapa hapa Dodoma.

Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa kushiriki michezo hii kwa kucheza lakini pia kwa kuishangilia timu yetu, karibuni sana imetolewa na Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* Mheshimiwa Kigwangalla. Hayo ndiyo matangazo niliyokuwa nayo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nielezee suala moja ambalo nadhani linaweza likaleta mkanganyiko kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba ukisoma Kanuni zetu kwenye Ibara ya 94(1) inaongelea kwamba katika Mkutano wake wa mwezi Oktoba - Novemba kila mwaka, kwa siku zisizopungua tano Bunge litakaa kama Kamati ya Mipango kwa madhumuni ya kufanya nini? Kwa madhumuni ya kujadili na kushauri Serikali kuhusu Mapendekezo ya Utekelezaji wa Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka unaofuata.

Kwa hali ya kawaida na ndiyo Kanuni imekaa hivyo, kazi hii huwa inafanyika katika Bunge la Oktoba na Novemba ndiyo Serikali inaleta, kwa sababu Bunge kama sehemu ya wadau tunaletewa hayo mapendekezo ya mpango ili sasa baada ya kuyapokea hayo mapendekezo ya Bunge na

Wadau wengine Serikali inayachukua kwenda kuyafanyia kazi na Kanuni hizi zinaitaka Serikali baada sasa ya kupokea mapendekezo ilete sasa Mpango na Mpango huo utakuja kuwasilishwa mbele ya Wabunge kabla ya kuja Dodoma, Dar es Salaam na utakapowasilishwa mwezi wa tatu au wa nne, Waziri atausoma tu na Waziri wa Fedha tena atatoa *statement* yake *of the annual financial statement* ambayo *basically* ndiyo *framework* yake ya bajeti.

Baada ya tukio hilo, kwa sababu ni kuwasilisha tu hakuna maswali au mjadala. Ikishapokelewa sasa, Katibu wa Bunge ndiye anapeleka kwa Kamati ya Bajeti, ndiyo inafanya uchambuzi wa Mpango huo sasa ili Bunge la Bajeti linapoanza na Kamati ya Bajeti inapowasilisha hotuba yake, itakuwa sasa imeuchambua Mpango kwa niaba ya Bunge; na ripoti yake ndiyo itakayowezesha kuona mapendekezo ya Mpango ulioletwa na Serikali ulivyokaa; Kamati ya Bajeti inasema nini kuhusiana na Mpango huo, lakini pia yatakayofuata mwishoni sasa, bajeti ya Serikali inapowasilishwa rasmi.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mtiririko wa Kanuni zetu. Bahati mbaya tu; na siyo bahati mbaya, kwa sababu ni tukio kubwa la Uchaguzi ndiyo maana hatukuweza kulifanya hilo. Bunge na Serikali ndiyo wakaona tutumie fursa hii ya Mkutano huu wa Bunge kuyaleta haya mapendekezo. Ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge mliomba mpewe semina ya siku tatu ambayo imefanyika kuwawezesha muelewe hasa ni nini ambacho kinaletwa na Serikali.

Leo hii ndiyo tunaanza rasmi. Serikali sasa imeshawasilisha hoja hii mbele ya Bunge letu ili sasa tuweze kuyajadili mapendekezo haya ili Serikali ipate fursa ya kuwasikia. Yale ambayo watadhani yanapendeza yaingizwe, watafanya hivyo ili mpango sasa urejeshwe Bungeni. Nimeona niyaseme hayo ili twende pamoja.

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa tena matangazo; na leo matangazo ni mengi jamani! Tuwe tunajitahidi kwa utaratibu, maana yanapaswa yawekwe hapa mezani ili kiti kinapomaliza tu kipindi cha maswali, yaweze kutolewa.

Waheshimiwa Wabunge, pia lipo tangazo kutoka Taasisi ya Uwekezaji ya UTT inaendelea kuwakaribisha Wabunge na Waheshimiwa Mawaziri wote, mpite na kujionea miradi mbalimbali ikiwemo uwekezaji kwenye masoko ya hisa pamoja na uuzwaji wa viwanja vya makazi na biashara. Wapo hapa kwenye viwanja vyetu, kwenye Jengo la Utawala pale nyuma.

Nilisema siku ile siyo kwa maana kwamba nawapigia pipa, hapana; mimi ni miongoni mwa watu walionufaika sana na vipande hivi. Nawashauri sana ni fursa nzuri sana. Mara nyingi Watanzania huwa tunalalamika sana, fursa ziko

wapi? Fursa zipo kwa wale wanaopenda kuzitumia. Na mimi nawahimiza sana Waheshimiwa Wabunge, tutumie fursa hizi. *(Makofi)*

Sasa nimemaliza matangazo, naendelea na utaratibu wetu. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ambayo ilipelekewa mapendekezo haya, tupate ripoti yao. *(Makofi)*

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo!

**MWENYEKITI:** Ehe, Mwongozo!

**MHE. JAMES K. MILLYA:** James Millya!

**MWENYEKITI:** Uko wapi?

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Huko! Huko hawapo.

**MWENYEKITI**: Uko wapi Mwongozo!

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo!

**MWENYEKITI:** Taja jina lako.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Jesca Kishoa.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Tundu Lissu!

**MWENYEKITI:** Aaah twende kwa utaratibu, wewe Mheshimiwa nani?

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni *Chief Whip*, hawa wengine wanatakiwa wanifuate baada ya mimi kuzungumza. *Yes! (Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Wewe sio Kiongozi wa Upinzani Bungeni, wewe ni Mbunge kama wengine ila mna utaratibu… *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *this is a Chief Whip!*

**MWENYEKITI:** Aah, Mheshimiwa jina lako nani?

**MHE. JAMES K. MILLYA:** James Millya!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto Kabwe! Nachukua majina tu. Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Jesca Kishoa.

**MWENYEKITI:** Millya na nani?

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Jesca Kishoa.

**MWENYEKITI:** Jesca Kishoa, Kubenea, *okay!* Tuanze na Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Juzi nimesimama hapa…

**MWENYEKITI:** Kanuni!

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Naam!

**MWENYEKITI:** Kanuni? *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa Kanuni ya 68(7), ni kanuni ya kuomba Mwongozo, inasema; "Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge yeyote anayesema, na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye kadri anavyoona inafaa." *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi jioni wakati ukiahirisha Bunge, uliamuru katika Bunge lako Tukufu waingizwe askari polisi na askari wa Bunge. Katika kitendo hicho, Wabunge wanawake walisachiwa, walitolewa kwa *escort* na walidhalilishwa na askari wa kiume, walivuliwa nguo zao za ndani…

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaa! *(Kicheko)*

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Wakavuliwa shanga zao!

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaa! *(Kicheko)*

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Wakavuliwa hereni! *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah! *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Muongo! *(Kicheko)*

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Wakavuliwa pete… *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Naomba utulivu Bungeni! Mheshimiwa Kubenea!

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Anatudhalilisha huyu! Taarifa! Taarifa! *(Kelele)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu.

Waheshimiwa Wabunge, ni lazima tuendelee kuheshimu Kanuni zetu, tuendelee kutumia lugha ya Kibunge. Sasa Mheshimiwa Kubenea, mimi nasema hivi kuhusiana na Mwongozo wako; kwanza naamini ulikuwepo siku ya Semina ya Kanuni za Bunge. Nilisimama baada ya wasilisho zuri sana la *paper* hiyo ya Kanuni ya Bunge. Kwenye eneo hili nilisimama nikauliza, jinsi ilivyoandikwa inaleta mkanganyiko sana; unaposema mapema; mapema lini? Ndiyo maana tulikubaliana kwamba eneo hili linyooshwe kwa kutumia maneno yale yale yaliyoko kwenye *paper* iliyowasilishwa kwenu. Mapema siku hiyo ndiyo itakuwa na maana sana Kanuni hii.

Sasa Mwongozo wangu ni kwamba ukitaka kutafuta mwongozo kwenye kanuni hii ya 68(7) lazima iwe ni mapema kwa siku hiyo. Huu ndiyo Mwongozo ninaoutoa.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, si ungeniacha nikamaliza basi!

**MWENYEKITI:** Unabishana na mimi sasa?

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Si uniache nimalize basi! Kwanini umenikata katikati? Si uniache niwasilishe halafu ndiyo utoe huo Mwongozo!

**MWENYEKITI:** Nimesimama bwana! Nimesimama! Naendelea sasa, iwapo hukubaliani na Mwongozo huu, tumia Kanuni, nenda kwenye Kanuni ya (5) utapata jibu. Mimi nisingependa kukae hapa naanza kuwafundisha utumiaji wa Kanuni, hapana, nahimiza mzitumie vizuri. Huo ndiyo mwongozo wangu kuhusiana na Mheshimiwa Kubenea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jesca!

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7), kwa sababu ya muda naomba nisiisome, lakini kwa ruhusa yako, naendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Mkurugenzi wa TAKUKURU ametangaza kwamba anawapeleka Mafisadi wakubwa Mahakamani wakiwemo mafisadi wa makontena. Kwa bahati mbaya sana, kinara mkubwa wa sakata la *Escrow,* Singh Seth pamoja na wale mafisadi ambao walibeba fedha kwenye malumbesa, hawajatajwa wala kufikishwa Mahakamani mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala wewe pia una maslahi nalo, lakini ni lazima tuseme kwa sababu fisadi huyu mpaka leo kila mwisho analipwa shilingi bilioni tano. Naomba Mwongozo wako, ni lini Serikali itachukulia hatua Maazimio ya Bunge lililopita mwaka mmoja uliopita la kufikisha mafisadi hawa mahakamani? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mmh!! Kwanza niseme kabisa kwa heshima zote, mwongozo wako uko nje kabisa ya Kanuni zetu. Tutaendelea kufundishana matumizi bora ya Kanuni hizi; lakini uko nje kabisa ya Kanuni. Naendelea. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa James Millya!

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(7) na kwa ruhusa yako naomba nisiisome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi wakati Mheshimiwa Kangi Lugola anauliza swali, alitoa maelekezo na akataja majina ili kuweka *clarity* kwenye swali lake. Naibu Spika anayefahamika kwamba ni *Ph.D holder* wa sheria, alimzuia kwa Kanuni ya 42 ambayo nimejaribu kuiangalia, haihusiki hata kidogo na namna ambavyo amemzuia. Lakini Kanuni ya 40(h), naomba niisome, inasema hivi; "linamtaja mtu yeyote kwa jina au kutoa maelezo mahsusi juu yake ila tu kama ni lazima ili kulifanya lieleweke." Alivyokuwa anafanya Mheshimiwa Kangi Lugola ni kuelezea ili kufundisha na kuiwezesha Serikali kufahamu ukweli juu ya mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba Mwongozo wako, kwa sababu hatutaki Bunge liburuzwe na tunyimwe haki ya kuleta *clarity* kwenye Bunge ili kuwafundisha Watanzania ukweli. Naomba Mwongozo wako, ahsante sana. Kwa sababu Kanuni aliyoinukuu sijaiona. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Millya nakushukuru sana. Hili nitalijibu hapa hapa, sasa hivi. La kwanza, kwa mujibu wa Kanuni zetu, Mwongozo au uamuzi ukishatolewa na Spika, Naibu Spika au yeyote ambaye yuko kwenye Kiti hiki, ni wa mwisho. *(Makofi)*

Wewe kama unaona una tatizo na hilo, ndiyo unatumia Kanuni hizo hizo ku-*challenge,* kuhoji uhalali wa uamuzi huo ili sasa Kamati ya Kanuni iende

ikalipokee hilo lalamiko na lifanyiwe kazi na uamuzi utoke. Ndiyo tunajenga *jurisprudence* ya kuimarisha Kanuni hizi matumizi yake.

La pili, kwa heshima zote Mheshimiwa Millya, sijui kama wewe umekuwa leo Wakili wa Mheshimiwa Mbunge wetu wa Mwibara! Sijui lakini… *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Ni Wakili wa Kanuni! *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ningetegemea hili, ungejielekeza tu bila hata kumtaja yeye, ungesema tu swali, je, kwa mujibu wa Kanuni hiyo, mimi natata tu nisaidiwe kuelewa. Maana swali la nyongeza ni swali. Ninyi Wanasheria mnajua kabisa, swali la nyongeza linatokana na swali la msingi. Naendelea, Mheshimiwa Zitto Kabwe!

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mfupi uliopita Waziri wa Fedha ametoa hotuba ya mapendekezo ya mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017); hajatoa hotuba ya mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2016/2017. Maelezo ambayo umeyatoa kutu-*guide* kwenye kuchangia ambapo umetumia kanuni ya 94(1) mapaka (4) ni maelezo yanayohusiana na Mpango wa Mwaka Mmoja; hayahusiani na Mpango wa miaka mitano. Tunajadili Mpango huu kwa masharti ya Katiba, Ibara ya 63 ya Katiba. Naomba niisome 63(3) (c); "Bunge kujadili na kuidhinisha Mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano na kutunga Sheria ya Kusimamia utekelezaji wa Mpango huo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, umetupa maelekezo hapa kwa Kanuni ya 94 ambayo inazungumzia Mpango wa mwaka mmoja mmoja. Kanuni ambazo unazitumia zinakukataza kuwahisha shughuli za Bunge. Hatujafikia bado, kwenye kujadili Mpango wa mwaka mmoja mmoja. Tunachokijadili sasa hapa ni Mpango wa miaka mitano ambao itabidi tuutungie Sheria halafu ndiyo tuje kwenye huo utaratibu ambao wewe unaueleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maelekezo yako yanakiuka Kanuni, hayajafuata utaratibu; na hapa ambapo Waziri ametusomea, Waziri hajatuletea Mpango. Waziri ameleta Mwelekeo wa Mpango. Bunge halitakiwi kujadili Mwelekeo wa Mpango. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuelewane katika hili. Hili ni suala la nchi yetu, siyo suala la vyama. Serikali mkiruhusu mjadili Mwelekeo wa Mpango, mnajidhalilisha! Mnapaswa mjadili Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu; na bahati nzuri wewe ulikuwa Mwanasheria wa muda mrefu, unapaswa kutungiwa sheria. Moja ya matatizo ya mpango uliopita kwamba haukutekelezwa, ni kwa sababu tulikosea, hatukutunga sheria. Leo mnataka kurudia yale yale! Hatuwezi kwenda. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuomba, hakuna cha kujadili hapa. Hakuna Mpango wa Maendeleo ambao umeletwa na Serikali, haupo! Maelekezo yako ni ya Mpango wa Mwaka. Bado, Umewahisha shughuli za Bunge!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba na kanuni zinakuruhusu. Kanuni ya 68...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, zingatia muda!

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uende kwenye Kanuni ya 68(5) kwa sababu najua jambo hili huwezi kuliamua wewe hapo sasa hivi; "Katika kufikia uamuzi wake, Spika aweza kuitaka Kamati ya Kudumu ya Kanuni za Bunge au Kamati nyingine yoyote ya Bunge impe ushauri kwenye jambo husika."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwombe Spika, mwende kwenye Kamati ya Kanuni ili mkajadili, kwa sababu Mpango wa Maendeleo wa Serikali haujaja hapa. Mkijadili Mwelekeo wa Mpango, mnaliua Bunge; halitakuwa limefanya kazi yake kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 63 (3)(c). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kwako! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, nimekusikia vizuri sana na Bunge limekusikia. Siwajibiki kukujibu moja kwa moja, acha nikalitafakari tu, nione mtiririko wa hoja yako na maelezo yangu ya awali. Maana siyo mara ya kwanza kwamba tunaanza kutekeleza Mpango wa miaka mitano, tunaingia *Phase II*. Umesema mengi, lakini acha tu nilichukue nikaone, nitafakari vizuri hayo ya kwako uliyoyasema, lakini najua tutaenda vizuri tu.

Waheshimiwa Wabunge, naendelea! Mwongozo wa mwisho, Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami sipo mbali sana na Mheshimiwa Zitto Kabwe, lakini naomba nianzie kwenye Orodha ya Shughuli za leo za Bunge lako Tukufu.

Orodha ya Shughuli za leo inaonyesha kwamba Waziri wa Fedha na Mipango atawasilisha Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kwa kipindi cha miaka mitano kinachoanzia 2016/2017 hadi 2020/2021. Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kwa kipindi hicho upo wapi? Haujawasilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili Kanuni ya 94(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu inasema; Bunge litakaa kama Kamati ya Mipango ili kukidhi matakwa ya Ibara ya 63 (3) (c) ya Katiba ambayo inasema: "Bunge litajadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unao kusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano na-*underline* kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo." Tutakaa kwa siku tano hapa, tutajadili na kuidhinisha Mpango, tutautungia sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba, Muswada wa Sheria husika uko wapi? Tutaupitisha lini? Muswada haupo, Mpango wa Pili wa Maendeleo, haupo. Tunajadili kitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, nimekusikia ukisema kwamba baada ya mjadala huu Kamati ya Bajeti ndiyo itakayopelekewa Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia shughuli za Kamati ya Bajeti, aya ya (9) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu. Labda mimi nina matatizo ya macho lakini ukurasa wa 138, nimejaribu kuangalia kazi za Kamati ya Bajeti zilizotajwa hapo sijaona mahali popote ambapo Kamati ya Bajeti ina mamlaka au ina majukumu ya kupokea na kujadili Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili Bunge lako Tukufu linahitaji kuongozwa sawasawa na nina wasiwasi kama unaelekeza Bunge hili sawasawa.

**MWENYEKITI:** Nakuomba uketi!

Mwongozo uliouomba kwangu unashabihiana na maombi ya Mwongozo yaliyotolewa na Mheshimiwa Zitto Kabwe. Maadam nimeshatoa mwongozo kwa hilo kwamba nalichukua nikalitafakari vizuri na ya kwako hayo yatakuja kujibiwa hivyo hivyo tu. Tutaenda vizuri tu.

Waheshimiwa Wabunge, mara nyingi huwa nawaomba sana, kila mmoja wetu ana *style* yake ya kuwasilisha hoja yake. Wengine tuna sauti kali kidogo, wengine za kati kati; ndivyo tulivyo.

Kwa hiyo, msiwe mnaona ajabu kama mtu anaongea kidogo na msisimko. Ndiyo *style* hizo. Nimekuwa *very fair* kwa wote kwa eneo hili la Mwongozo ili twende na muda wetu tumeuminya kidogo.

Sasa namwita Mwasilishaji wetu wa pili ambaye atakuwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, kwa muda huo huo wa dakika 30, karibu Mwenyekiti, Mheshimiwa Hawa Ghasia!

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Hoja ya kuahirisha mjadala, Kanuni ya 69.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto Kabwe, nimeshaliamulia hilo na nikimwita mwenye hoja ambaye ndiye Waziri, tulimwita, soma Kanuni ya 52. Huu ni mtiririko, unaanzia Kanuni ya 52, endelea Mwenyekiti.

**MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 94 (5) ya Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la 2016, naomba kuchukua fursa hii kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Taifa wa miaka mitano 2011/2012 hadi 2015/2016 pamoja na Mwelekeo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha miaka mitano 2016/2017 hadi 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu tulivyopata Uhuru mwaka 1961 agenda ya maendeleo imekuwa ikiweka msukumo mkubwa hasa katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini na hivyo kuhakikisha kuwa Watanzania walio wengi wananufaika na maendeleo yanayopatikana. Katika kipindi chote hicho, Serikali imekuwa ikiandaa na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya muda wa kati na muda mrefu ikiwemo ile iliyolenga kupambana na maadui wakuu wa maendeleo ya Taifa, yaani umaskini, ujinga na maradhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushindwa kutekelezwa kwa programu mbalimbali za kufufua na kurekebisha uchumi kulipelekea mwaka 1999 kuwa na Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025 yenye lengo la kuiwezesha Tanzania kubadili mfumo wa uchumi wake na kuiwezesha nchi kufikia hadhi ya nchi zenye uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Utekelezaji wa dira hii umepelekea kuwa na Mipango ya Maendeleo ya miaka mitano mitano; Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa ukiwa ni wa mwaka 2011/2012 hadi 2015/2016 uliokuwa na dhima ya kufungua fursa za ukuzaji wa uchumi wa Taifa ambao leo tunatathmini utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili, Bunge lako Tukufu limepokea Muundo wa Mwelekeo wa Mpango wa Pili wa Taifa wa miaka mitano 2016/2017 hadi 2020/2021 wenye dhima ya kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kuwa Bunge lako Tukufu la Kumi na Moja ndilo lenye wajibu wa kusimamia ipasavyo utekelezaji wa mpango huu ili nchi yetu iweze kufikia malengo iliyojiwekea, Kamati ya Bajeti imefanya uchambuzi wa kina kuhusu tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo na huu tunaotegemea kuanza kuutekeleza ili kuweza kulisaidia Bunge lako Tukufu kupata taswira ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza na mwelekeo wa utekelezaji wa Mpango wa Pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya Kamati inaonyesha Pato la Taifa kwa kipindi hicho lilikua kwa wastani wa asilimia 6.7 pungufu kidogo ya lengo lililokusudiwa la asilimia nane. Sekta zilizochangia ukuaji huo kwa kiasi kikubwa ni mawasiliano ambayo ilikuwa kwa asilimia 15.3; ujenzi, asilimia 13; huduma za kijamii, asilimia 9.9 na usafirishaji asilimia 8.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto bado ipo kwenye sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na misitu ambazo zinatoa ajira kwa Watanzania walio wengi. Sekta hizo zilikuwa chini ya asilimia nne na hivyo kushindwa kufikia lengo la asilimia sita kama lilivyoainishwa kwenye Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Taifa na hivyo kushindwa kuchangia vyema ukuaji wa Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uchumi kukua, takwimu zinaonyesha kwamba hali ya umaskini wa kipato imeendelea kuwa kubwa katika maeneo ya vijijini ambapo ipo asilimia 33 kuliko mijini ambapo imeshuka hadi asilimia 21.7. Hali hii inaashiria kuwa ukuaji wa uchumi haujaweza kuboresha hali ya maisha ya wananchi wengi waliopo vijijini wenye kipato cha chini. Changamoto iliyopo kwa Serikali ni kuangalia namna gani mafanikio haya ya ukuaji wa uchumi mpana yanawafikia wananchi walio wengi vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa mfumuko wa bei katika kipindi hicho uliendelea kupungua na kuwa katika kiwango cha tarakimu moja. Takwimu za Serikali zinaonyesha kwamba mwaka 2015 mfumuko wa bei uliendelea kuwa chini ya lengo la muda wa kati la asilimia tano ikilinganishwa na wastani wa mfumuko wa bei wa asilimia 5.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla mfumuko wa bei umeshuka kutoka asilimia 16.2 mwaka 2012 hadi asilimia tuliyoitaja. Hii inatokana na kupatikana kwa umeme wa uhakika na kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumuko wa bei mwaka 2012 ulikuwa juu kutokana na kutokuwepo kwa umeme wa uhakika ambapo kulipelekea gharama za uzalishaji viwandani pamoja na kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia ambapo kwa kiasi kikubwa sasa hivi vimeanza kutengemaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho, takwimu za Benki Kuu ya Tanzania zinaonesha kuwa kati ya kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015 thamani ya shilingi katika soko la mabenki imeendelea kushuka ikilinganishwa na dola ya Kimarekani. Wastani umeonyesha kuwa thamani ya shilingi kwa dola ya Kimarekani ilishuka kutoka shilingi 1,401.79 mwaka 2010 hadi shilingi 1,634.30 mwaka 2014; hadi kufikia mwezi Machi, 2015 thamani ya shilingi ilishuka kwa asilimia 9.6 katika soko la jumla na asilimia 13 katika soko la rejareja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kiuhalisia kwa sasa dola ya Kimarekani inabadilishwa kwa shilingi 2,000/=. Upunguaji wa thamani ya shilingi ya Tanzania unaathiri sana utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na uchumi wa nchi.

Kwanza, kwa upande wa kuagiza bidhaa nje na hivyo kusababisha mfumuko wa bei, yaani *imported inflation*.

Pili, kuongeza mzigo wa malipo ya mikopo ya nje kwa mikopo ya Serikali na Sekta binafsi; na tatu, kupunguza uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati iliangalia mwenendo wa mapato na matumizi ya Serikali. Katika kipindi hiki bajeti ya Serikali imekuwa ikikua mwaka hadi mwaka kutoka shilingi trilioni 11.6 mwaka 2010/2011 hadi shilingi trilioni 19.8 mwaka 2014/2015. Kwa kipindi chote cha miaka mitano, utekelezaji wa bajeti ya Serikali haujawa wa kuridhisha. Kiasi cha mapato kinachokusanywa kimekuwa hakikidhi matumizi ya Serikali na hivyo kupelekea nakisi ya bajeti kwa miaka yote mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imesababisha Serikali kutegemea mikopo ya ndani na nje ya nchi ili iweze kukidhi bajeti yake na hivyo kushindwa kufikia lengo la asilimia 35 ya bajeti inayotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Changamoto kubwa iliyopo ni kwamba matumizi ya Serikali hufanyika nje ya bajeti iliyotengwa wakati makadirio ya makusanyo ya kodi kuwa chini ukilinganisha na zaidi ya uwezo halisi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi, 2015 deni la Serikali lilikuwa dola za Kimarekani bilioni 19.5 sawa na shilingi trilioni 35. Kati ya fedha hizi, deni la nje ni shilingi trilioni 25.6 na deni la ndani ni shilingi trilioni 9.4. Kielelezo hapo chini kinaonyesha kuwa deni la ndani linazidi kuongezeka tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni la ndani linaongezeka kutokana na Serikali kushindwa kufikia malengo ya ukopeshwaji katika soko la nje, hivyo kulazimika kukopa katika soko la ndani pia huongezeka kwa ubadilishwaji wa hati za

ukwasi kugharamia matumizi ya Serikali. Hii imetokana na makusanyo ya mapato kuendelea kutokidhi matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika soko la ndani, Benki za Kibiashara zinaongoza kumiliki sehemu kubwa ya deni la ndani kwa kiwango cha asilimia 51.5, Benki Kuu inamiliki kwa asilimia 21.1 na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa asilimia 15.1, Bima asilimia saba na wadau wengine asilimia zilizobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwiano wa amana na fedha za kigeni pamoja na uwiano kati ya amana na riba za mikopo vimeendelea kushuka. Ukuaji wa mkopo kwa sekta binafsi ulifikia wastani wa asilimia 19.9 katika kipindi cha miaka mitano. Hii ni sawa na asilimia 20.9 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu kubwa ya mikopo ya sekta binafsi ilielekezwa katika shughuli za biashara ikifuatiwa na shughuli binafsi, viwanda na mwisho kilimo. Mwenendo wa ukopaji kwenye vyanzo vya ndani unaonyesha kuwa katika kipindi cha miaka mitano Serikali imejitahidi kukopa katika kiwango cha asilimia moja ya pato la Taifa kinachotakiwa. Changamoto kubwa bado ipo kwenye upande wa riba zinazotozwa na mabenki kuwa kubwa sana hivyo kuongeza gharama za ukopaji kwa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapaswa kuongeza kasi ya kufanya maboresho katika sekta ya fedha na kuweka mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na kuimarisha Vyama vya Ushirika ili kutoa fursa kwa wananchi kupata mikopo kwa riba nafuu.

Hadi mwezi Aprili, 2015, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Kimarekani milioni 4,043.4 sawa na shilingi bilioni 7,338.7 zinazotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 3.9. Serikali inashauriwa kuongeza kiwango cha akiba ya fedha za kigeni ambacho kitatosheleza kwa kipindi kisichopungua miezi sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kielelezo kilichopo kinaonesha utekelezaji wa malengo makuu ya viashiria vya uchumi katika Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano. Malengo ya mpango wa kwanza yalikuwa ni kutanzua vikwazo vya kiuchumi, kupunguza umaskini na kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii. Malengo haya yote yalielekezwa katika kutekeleza maeneo ya vipaumbele ambavyo ni miundombinu; reli, barabara, bandari, usafiri wa anga na nishati, kilimo, mazao, mifugo, uwindaji, misitu na uvuvi, viwanda, madini, maendeleo ya rasilimali watu na huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti ilichambua kwa kina utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele, kwa kila sekta kwa kuangalia upatikanaji wa fedha kwa kila kipaumbele, muda wa kati na muda mrefu wa utekelezaji wa kila

kipaumbele na uwajibikaji wa wataalam wa sekta husika katika kila kipaumbele. Mchanganuo huo umetoa picha halisi ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hii Kamati ya Bajeti inatoa tathimini yake ya utekelezaji wa vipaumbele vya sekta kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nchi ipige hatua ya maendeleo, basi ni dhahiri, lazima iwe na miundombinu ya uhakika ya kuweza kukidhi mahitaji mbalimbali ya usafiri wa malighafi na bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imepitia malengo makuu yaliyowekwa katika maeneo ya reli, barabara, bandari na usafiri wa anga na kugundua kuwa kwa ujumla Serikali imeshindwa kufikia baadhi ya malengo yake makuu kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2011/2012 hadi 2015/2016. Baadhi ya maeneo yapo chini ya lengo la utekelezaji kwa 50% na hii imechangiwa sana na kutokupatikana kwa rasilimali fedha kwa wakati au kutokupatikana kabisa kwa fedha za kugharamia miradi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni reli ya kati; lengo la Mpango lilikuwa ifikapo mwaka 2015 Serikali itakuwa imekarabati kilomita 2,707 za reli ya kati, lakini mpaka sasa ni kilomita 136 tu za reli ndizo zimekarabatiwa. Aidha, sura tuliyoitoa kwenye miradi ya reli ndiyo tunayoiona kwenye miradi ya nishati na miradi ya barabara na miradi ya bandari na usafiri wa anga. Lengo kubwa la Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Taifa lilikuwa ni kuongeza ukuaji wa Sekta ya Kilimo kutoka 2.7% mwaka 2010 hadi ifikapo mwaka 2015. Hata hivyo lengo hili limeshindwa kufikiwa, limefikiwa kwa chini ya 4%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya sekta ya kilimo ipo nje ya malengo tuliyojiwekea na hasa kwa upande wa uzalishaji wa mazao ya thamani yaani mifugo na uvuvi. Changamoto bado ipo katika kuongeza maeneo ya umwagiliaji na usimamizi thabiti wa upotevu wa misitu pamoja na ukuaji wa sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uvuvi imekua kutoka 0.9% mwaka 2010 hadi asilimia 2%. Malengo Makuu ya Mpango wa Kwanza wa maendeleo yalikuwa ni kuhakikisha kuwa sekta hii inakuwa kwa 11% ifikapo 2015/2016. Mpaka sasa lengo hili halijafikiwa kwani hadi kufikia mwaka 2014 sekta hii imekua kwa 8% tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ambayo tumeangalia tumefanyia tathmini ni sekta ya madini, maendeleo ya rasilimali watu pamoja

na mapitio ya Sera ya Kuondoa Umaskini na suala zima la utekelezaji wa MKUKUTA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti imepitia na kuchambua kwa kina mapendekezo ya muundo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa unaounganishwa na mkakati wa kukuza uchumi na kuondoa umaskini Tanzania ambao una dhana ya kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Kamati inatambua lengo la Mpango huu na ule uliopita ni kuhakikisha Tanzania inakuwa nchi yenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2020/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti inakubaliana kuunganisha Mpango wa Maendeleo pamoja na MKUKUTA ili kuwianisha ajenda ya kupunguza umaskini katika Mipango ya Maendeleo. Hatua ya kuunganisha itasaidia kutatua changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa MKUKUTA na Mpango kwa pamoja na hivyo kutanzua changamoto za kiutekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inakubaliana na Serikali kuhusisha kwa jitihada nyingine ambazo zilikuwepo chini ya Mpango wa Kwanza wa miaka mitano kama vile Matokeo Makubwa Sasa, Mpango Mama wa Kutathmini Umaskini na Malengo ya Maendeleo Endelevu kwenye Muundo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa miaka mitano wa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti inashauri kuwa ni vyema vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo uliopita ambavyo havijatekelezwa vikahuishwa kwenye Mpango huu mpya ili kuhakikisha kuwa, dhana ya kufungulia fursa za ukuaji wa uchumi wa Taifa inafungamana na dhana mpya ya kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa ukuaji wa uchumi unaonesha kuwa unategemea zaidi sekta ya huduma kuliko sekta ya uzalishaji kama kilimo na viwanda. Mwenendo huu sio endelevu kuweza kukidhi na kuleta maendeleo tarajiwa ya kuondoa umaskini wa kipato.

Kamati inapendekeza kuwa muundo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ujikite zaidi katika sekta za kilimo na viwanda vinavyochakata mazao ya kilimo pamoja na masoko yake. Uzoefu unaonesha kuwa uchumi unaotegemea viwanda unashamiri pale ambapo sekta ya kilimo inakuwa endelevu na inayojitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeainisha maeneo na mikakati mbalimbali ikiwemo sekta binafsi kushiriki katika kugharamia Mpango wa Pili wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado sekta binafsi nchini inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo kwa namna moja au nyingine zitaathiri ushiriki wao kikamilifu katika kuchangia pato la kugharamia mpango husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuyafanyia marekebisho maeneo mbalimbali yanayohusu sekta binafsi kama ifuatavyo:-

(1) Kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini yaani *doing business and investment climate,* kwani Tanzania imekuwa ikishika nafasi ya 128 hadi 131 kati ya nchi zenye mazingira wezeshi ya uwekezaji na ufanyaji biashara.

(2) Serikali ihakikishe kuwa sheria zinazosimamia masuala ya uwekezaji zinakuwa thabiti na zisizobadilika mara kwa mara. Mfano, kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2009 hadi 2015, Sheria ya Uwekezaji imebadilishwa takribani mara sita, hivyo inaonesha kwamba sheria na sera zetu za uwekezaji hazipo thabiti na endelevu.

(3) Serikali ifanye mapitio ya sera na sheria ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi ya mwaka 2010.

(4) Pia Serikali ianze kufikiria kujiondoa kwenye utaratibu wa kukopa katika taasisi za fedha na mabenki ya ndani ambayo unasababisha sekta binafsi kukopa mikopo kutoka vyanzo vya ndani vya fedha. Hivyo, kutopata mikopo kutoka vyanzo vya ndani na hivyo kuathiri ushiriki wao.

(5) Sekta ya umma ndio mdau mkubwa katika utekelezaji wa Mpango wa Pili, hivyo ni vema ikatatua changamoto zinazoikabili katika ukusanyaji wa mapato ili iweze kugharamia Mpango wa Maendeleo.

(6) Serikali pia ni lazima iondokane na kutegemea mikopo na misaada ya kutoka nje na badala yake iimarishe ukusanyaji wa mapato ya ndani kwani ndio chanzo cha uhakika.

(7) Serikali inatakiwa kuziba mianya yote ya rushwa katika ukusanyaji wa mapato.

(8) Serikali ipunguze matumizi ya hati fungani katika kuziba nakisi ya bajeti kwani kutokana na ufinyu wa soko la mitaji mara nyingi wanunuzi wakubwa hati fungani ni mabenki na taasisi za fedha zilizo chini. Hatua hiyo hupunguza ukwasi

zaidi wa taasisi za mabenki ambazo zingetumika kutoa mikopo kwa sekta binafsi.

(9) Serikali ichukue hatua madhubuti na makusudi kuhakikisha kwamba Watanzania wanakuwa na utamaduni wa kuweka akiba ili uongeze upatikanaji wa mikopo kwa watu binafsi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ya kipaumbele ya Mpango wa Pili kwa Maendeleo, eneo mojawapo lililoainishwa ni sekta ya miundombinu hasa upande wa reli, barabara, bandari na usafiri wa anga.

Kamati ya Bajeti inashauri kwamba maendeleo ya viwanda yaliyokusudiwa kutekelezwa, yazingatie uboreshaji wa miundombinu hasa kwa upande wa upanuzi wa bandari, miradi ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa, mpango wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo utakaowasilishwa hapo baadaye uoneshe muda na gharama za utekelezaji wa miradi husika. Aidha, Serikali iimarishe vitengo vya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi itakayoainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya jumla, Kamati ya Bajeti inatoa ushauri wa ujumla kama ifuatavyo:-

(1) Kuhuisha sheria zote zinazohusiana na masuala ya uwekezaji nchini.

(2) Kuhuishwa kwa sheria hizi kutahamasisha sekta binafsi kutoka ndani na nje ya nchi kushiriki katika utekelezaji wa mpango kwa sababu taratibu za uwekezaji katika sekta mbalimbali zitakuwa chini ya mwamvuli mmoja.

(3) Kukamilisha tathmini ya uwezo wa kukopa na kulipa ili kupanua wigo wa sekta binafsi na Serikali kukopa katika vyanzo vya fedha vya nje.

(4) Serikali ihakikishe kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya kulipa fidia na utengenezaji wa miundombinu ya msingi kwenye maeneo mbalimbali na hasa ile ya miradi mikubwa ya kielelezo zinapatikana kwa wakati uliopangwa.

(5) Serikali ihakikishe upatikanaji wa rasilimali watu wenye ujuzi, uwezo na taaluma ya kufanya kazi katika sekta mbalimbali za uchumi itakayokuwa chachu ya kuleta matokeo thabiti na endelevu katika sekta husika.

(6) Serikali iendelee kusimamia suala la uadilifu na uwajibikaji wa watumishi wa sekta ya umma na sekta binafsi kwa kuzingatia sheria, kanuni na

taratibu zilizopo katika masuala ya ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yangu yote iingizwe kwenye *Hansard* kama ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda nimshukuru Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, na Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Ashatu Kijaji kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia wataalam wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili muundo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali yaliyohusu muundo wa mpango husika na napenda niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdalah, Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mheshimiwa Maria Kangoye, Mheshimiwa Suzan Masele, Mheshimiwa Augustino...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo tulishakubaliana siku za nyuma.

**MHE. HAWA A. GHASIA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KWANZA WA MAENDELEO YA TAIFA WA MIAKA MITANO 20112012 – 2015/2016 PAMOJA NA MWELEKEO WA MPANGO WA PILI WA MAENDELEO WA TAIFA KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO 2016/2017–2020/2021 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 94(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2016 naomba kuchukua fursa ili kuwasilisha Taarifa ya

Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16) pamoja na Mwelekeo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha Miaka Mitano (2016/17-2020/21).

**Mheshimiwa Spika**, Tangu tulivyopata uhuru mwaka 1961, ajenda ya maendeleo imekuwa ikiwekewa msukumo mkubwa hasa katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini; na hivyo kuhakikisha kuwa watanzania walio wengi wananufaika na maendeleo yanayopatikana. Katika kipindi chote hicho Serikali imekuwa ikiandaa na kutekeleza mipango ya maendeleo ya muda wa kati na mrefu ikiwemo ile iliyolenga kupambana na maadui wakuu wa maendeleo ya taifa yaani umaskini ujinga na maradhi.

**Mheshimiwa Spika**, Kushindwa kwa utekelezaji wa program mbalimbali za '***kufufua na kurekebisha uchum***i' kulipekea mwaka 1999; kuwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 (mpya) yenye lengo la kuiwezesha Tanzania kubadili mfumo wa uchumi wake na kuiwezesha nchi ifikapo mwaka 2025 tuwe tumefikia hadhi ya nchi zenye uchumi wa kipato cha kati. Utekelezaji wa Dira hii umepelekea kuwa na Mipango ya maendeleo ya miaka mitano mitano; Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa (2011/12-2015/16) uliokuwa na dhima ya '***kufungulia fursa za ukuaji wa uchumi wa Taifa'***; ambao leo tunatathmini utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, Sambamba na hili, Bunge lako tukufu limepokea muundo wa mwelekeo wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) wenye dhima ya '***kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu'.*** Kwa kuzingatia kuwa Bunge lako Tukufu la 11 ndio lenye wajibu wa kusimamia ipasavyo utekelezaji wa Mpango huo ili nchi yetu iweze kufikia malengo iliyojiwekea. Kamati ya Bajeti imefanya uchambuzi wa kina kuhusu tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa kwanza wa Maendeleo na huu tunaotegemea kuanza kuutekeleza ili kuweza kulisaidia Bunge lako tukufu kupata taswira ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza na mwelekeo wa utekelezaji wa Mpango wa Pili.

## 2.0 TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KWANZA WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2011/12-2020/21)


### 2.1 Mapitio ya Mwenendo wa Uchumi jumla

#### 2.1.1 Ukuaji wa Pato la Taifa

**Mheshimiwa Spika**, Tathmini ya Kamati inaonyesha Pato la Taifa katika kipindi hicho lilikua kwa wastani wa asilimia 6.7; pungufu kidogo ya lengo lililokusudiwa la asilimia 8. Sekta zilizochangia ukuaji huo kwa kiasi kikubwa ni mawasiliano (asilimia 15.3); ujenzi (asilimia 13.0); huduma za fedha (asilimia 9.9) na usafirishaji (asilimia 8.8). Changamoto bado ipo kwenye, Sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na misitu ambazo zinatoa ajira kwa Watanzania walio wengi; hazijafanya vizuri katika kuchangia ukuaji wa Pato la Taifa. Sekta hizo zilikua chini ya asilimia 4 na hivyo kushindwa kufikia lengo la asilimia 6 kama lilivyoainishwa kwenye Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uchumi kukua, takwimu zinaonyesha kwamba hali ya umaskini wa kipato imeendelea kuwa kubwa hasa katika maeneo ya vijijini (asilimia 33) kuliko mjini ( asilimia 21.7). Hali hii inaashiria ukuaji wa uchumi haujaweza kuboresha hali ya maisha ya wananchi wengi waliopo vijijini wenye kipato cha chini. Changamoto iliyopo kwa Serikali ni kuangalia namna gani mafanikio haya ya ukuaji wa uchumi mpana yanawafikia wananchi wengi walio vijijini.

**Kielelezo Namba 1: Mwenendo wa ukuaji wa uchumi kwa kipindi cha mwaka 2010/11 hadi 2014/15**



Chanzo: Wizara ya Fedha

### 2.1.2 Mwenendo wa mfumuko wa bei na thamani ya Shilingi

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa mfumuko wa bei katika kipindi hicho uliendelea kupungua na kuwa katika kiwango cha tarakimu moja. Takwimu za Serikali zinaonyesha kwamba kwa mwaka 2015, Mfumuko wa bei uliendelea kuwa chini ya lengo la muda wa kati la asilimia 5 ikilinganishwa na wastani wa mfumuko wa bei asilimia 5.4 kwa Mwaka 2014 na wastani asilimia 7.9 kwa mwaka 2013. Mwaka 2012 Mfumuko wa bei ulikuwa katika kiwango cha tarakimu mbili (asilimia 16.2) hii ilitokana na kutopatikana kwa umeme wa uhakika uliopelekea kuongezeka kwa gharama za uzalishaji viwandani pamoja na kupanda kwa bei ya mafuta kwenye soko la dunia.


**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hicho, Takwimu za Benki kuu ya Tanzania zinaonyesha kuwa kati ya kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015; thamani ya shilingi katika soko la mabenki imeendelea kushuka ukilinganisha na Dola ya Kimarekani. Wastani umeonesha kuwa thamani ya shilingi kwa dola za kimarekani ilishuka kutoka shilingi 1,401.79 mwaka 2010 hadi hadi shilingi 1,634.3 mwaka 2014. Hadi kufikia mwezi machi 2015, thamani ya shilingi ilishuka kwa kasi kwa asilimia 9.6 katika soko la jumla na asilimia 13.0 katika soko la rejareja na hivyo kupelekea dola moja kubadilishwa kwa wastani wa shilingi 1,786.3 hata hivyo kiuhalisia kwa sasa inabadilishwa kwa zaidi ya shilingi 2000. Upunguaji wa thamani ya shilingi ya Tanzania unaathiri sana utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na uchumi wa nchi; kwanza, katika upande wa kuagiza bidhaa nje (import bill) na hivyo kusababisha mfumuko wa bei (imported inflation); pili, kuongeza mzigo wa malipo ya mikopo ya nje kwa mikopo ya Serikali na sekta binafsi; na tatu, kupunguza uwekezaji nchini.

### 2.1.3 Mwenendo wa Mapato na matumizi ya Serikali

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki bajeti ya Serikali imekuwa ikikua mwaka hadi mwaka kutoka shilingi trilioni 11.6 kwa mwaka 2010/2011 hadi shilingi trilioni 19.8 kwa mwaka 2014/15. Kwa kipindi chote cha miaka mitano, utekelezaji wa bajeti ya Serikali haujakuwa wa kuridhisha. Kiasi cha mapato kinachokusanywa kimekuwa hakikidhi matumizi ya Serikali na hivyo kupelekea nakisi ya bajeti kwa miaka yote mitano (budget deficit). Mfano kwa mwaka 2010/11 nakisi ya bajeti ilikuwa asilimia 8.4 ya Pato la Taifa; kwa mwaka 2011/12 ilikuwa 6.7 ya Pato la Taifa; kwa mwaka 2012/13 ilikuwa asilimia 5.4 ya Pato la Taifa; kwa mwaka 2013/14 ilikuwa


asilimia 8.1 ya Pato la Taifa na mwaka 2014/15 ilikuwa asilimia 9.2 ya Pato la Taifa. Hii imesababisha Serikali kutegemea mikopo ya ndani na nje ya nchi ili iweze kukidhi bajeti yake na hivyo kushindwa kufikia lengo la asilimia 35 ya bajeti inayotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Changamoto kubwa iliyopo kuwa matumizi ya Serikali kufanyika nje ya bajeti iliyotengwa wakati makadirio ya makusanyo ya kodi kuwa chini ya zaidi ya uwezo wa Serikali.

**Kielelezo Namba 2: Mwenendo wa Makusanyo ya Mapato ya Serikali: 2010/11-2014/15**




Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

**Kielelezo Namba 3 : Uwiano wa Pato la Taifa na Matumizi: 2010/11 hadi 2014/15**





Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

### 2.1.4 Deni la Taifa

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi, 2015 Deni la Taifa lilikuwa dola ya Marekani bilioni 19.5 sawa na shilingi trilioni 35. Kati ya fedha hizi

deni la nje ni shilingi trilioni 25.6 (sawa na asilimia 73.2) na la ndani ni shilingi trilioni 9.4 (sawa na asilimia 26.8). Kielelezo hapo chini kinaonyesha kuwa Deni la Ndani linazidi kuongezeka tofauti na ilivyokuwa hapo awali (2009/10). Deni la ndani linaongezeka kutokana na Serikali kushindwa kufikia malengo ya ukopeshwaji katika soko la nje hivyo kulazimika kukopa katika soko la ndani pia kuongezeka kwa ubadilishwaji wa hati za ukwasi (liquidity papers) kugharamia matumizi ya Serikali. Hii imetokana na na makusanyo ya mapato kuendelea kutokidhi matumizi ya Serikali. Katika soko la ndani, benki za biashara zinaongoza kumiliki sehemu kubwa ya deni la ndani kwa kiwango cha asilimia 51.5; benki kuu inamiliki asilimia 21.1; mifuko ya hifadhi asilimia 15.1; Bima asilimia 7 na wadau wengineo asilimia 3.4 ya deni la ndani la Taifa.

**Kielelezo Namba 4: Mwenendo wa ukuaji wa Deni la Taifa kwa kipindi cha mwaka 2009/10 hadi 2014/15.**




| | Deni la Ndani | Deni la Nje | Jumla ya Deni la Taifa |
|---|---|---|---|
| 2009/10 | 2,254 | 7,858 | 10,112 |
| 2010/11 | 3,707 | 10,735 | 14,442 |
| 2011/12 | 4,076 | 12,430 | 16,506 |
| 2012/13 | 5,775 | 15,634 | 21,409 |
| 2013/14 | 7,144.50 | 19,343 | 26,487 |
| 2014/15 | 9,400 | 25,600 | 35,000 |

Chanzo: Wizara ya Fedha

### 2.1.5 Huduma za kibenki na viwango vya riba

**Mheshimiwa Spika**, uwiano wa amana na fedha za kigeni pamoja na uwiano kati ya amana na riba za mikopo vimeendelea kushuka. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulifikia wastani wa asilimia 19.9 katika kipindi cha miaka miaka mitano (2010/11-2014/15), hii ni sawa na asilimia 20.9 ya Pato la Taifa. Sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi ilielekezwa katika shughuli za biashara, zikifuatiwa na shughuli binafsi, viwanda na mwisho kilimo. Mwenendo wa ukopaji kwenye vyanzo vya ndani (domestic borrowing) unaonyesha kuwa katika kipindi cha miaka mitano Serikali imejitahidi kukopa katika kiwango cha asilimia 1 ya Pato la Taifa

kinachotakiwa. Changamoto kubwa bado ipo kwenye upande wa riba zinazotozwa na mabenki zimeendelea kuwa kubwa sana hivyo kuongeza gharama za mikopo kwa miradi ya maendeleo. Benki zetu nyingi zipo katika mfumo wa kibiashara na hivyo inakuwa ni vigumu kukopesha mikopo ya muda mrefu na yenye riba nafuu. Mfano, katika kukopesha wakulima kwenye sekta ya kilimo; Serikali inahitajika kuongeza kasi ya kufanya maboresho katika sekta ya fedha na kuweka mazingira wezeshi ikiwa pamoja na kuimarisha vyama vya ushirika ili kutoa fursa kwa wananchi kupata mikopo kwa riba nafuu.

### 2.1.7 Akiba ya fedha za kigeni

**Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili 2015 akiba ya fedha za kigeni ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 4,043.4, zinazotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 3.9. Serikali inashauriwa kuongeza kiwango cha akiba ya fedha za kigeni ambacho kitatosheleza kwa kipindi kisichopungua miezi 6.

**Kielelezo Namba 5. Jedwali kuonyesha utekelezaji wa Malengo Makuu ya viashiria vya Uchumi katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16)**

| Na. | Eneo husika | Lengo | Mwenendo waUtekelezaji | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ukuaji wa Uchumi | Ufikie asilimia 8 | Umefikia wastani wa asilimia 6.7 | Chini ya lengo |
| 2 | Mazingira wezeshi ya ufanyaji Biashara duniani | Kupungua kuwa Chini ya nafasi ya 100 | Ni nchi ya 131 (Mwaka2015) | Chini ya lengo |
| 3 | Mchango wa Sekta ya uzalishaji Viwandani kwenye Pato la Taifa | Kuongezeka ufikie asilimia 12.9 | Imefikia asilimia 7 | Chini ya lengo |
| 4 | Ajira katika sekta ya uzalishaji viwandani | Ikue kutoka watu 120,000 mpaka zaidi ya 221,000 | Imekuwa na kufikia Watu 615,323 | Juu ya lengo |
| 5 | Udahili wa wanafunzi ktk ngazi Mbali mbali za vyuo | Uongezeke kutoka asilimia 1.5 mpaka asilimia 5 | Umeongezeka hadi Kufikia asilimia 4 kwa mwaka 2012 | Juu ya lengo |
| 6 | Uchangiaji wa sekta ya Madini Kwenye Pato la Taifa | UfikieaAsilimia 3.7 | Umefikia asilimia 3.7 kwa mwaka 2013 | Chini ya kiwango |
| 7 | Uchangiaji wa sekta ya Uvuvi Kwenye Pato la Taifa | Ufikie asilimia 5 | Umefikia asilimia 2.3 hadi kufikia mwaka 2013 | Chini ya kiwango |
| 8 | Wigo wa ufanyaji biashara katika soko la Dunia | Uongezeke kutoka 0.022 asilimia hadi 0.1 asilimia | Imefikia asilimia 0.016 hadi kufikia mwaka 2014 | Chini ya Kiwango |
| 9 | Mchango wa biashara kwenye Pato la Taifa | Kutoka asilimia 16 hadi kufikia asilimia 20 kwa mwaka 2015/16 | Hadi kufikia mwaka 2014 imechangia asilimia 19 | Kwa makadirio kiwango kimefikiwa |

## 2.2 Tathmini ya utekelezaji wa sekta zilizopewa kipaumbele kwenye Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Taifa (2011/12-2015/16).

**Mheshimiwa Spika**, malengo ya Mpango wa Kwanza yalikuwa ni kutanzua vikwazo vya kiuchumi, kupunguza umaskini na kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii. Malengo haya yote yalielekezwa katika kutekelezaji maeneo ya vipaumbele ambavyo ni Miundombinu (Reli, barabara, bandari, usafiri wa anga na nishati); Kilimo (mazao, mifugo, uwindaji, misitu na uvuvi); viwanda; madini; maendeleo ya rasilimali watu na huduma za jamii (afya, elimu na maji).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti ilichambua kwa kina utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele kwa kila sekta kwa kuangalia upatikanaji wa fedha kwa kila kipaumbele; muda wa kati na mrefu wa utekelezaji wa kila kipaumbele;na uwajibikaji wa wataalamu wa sekta husika katika kila kipaumbele. Mchanganuo huu umetoa picha halisi ya utekelezaji wa Mpango wa kwanza wa Maendeleo mpaka sasa. Kwa mantiki hii, Kamati ya Bajeti inatoa tathmini yake ya utekelezaji wa vipaumbele vya kisekta kama ifuatavyo:

### 2.2.1 Sekta ya Miundombinu

**Mheshimiwa Spika**, ili nchi ipige hatua ya maendeleo basi ni dhahiri lazima iwe na miundombinu ya uhakika ya kuweza kukidhi mahitaji mbalimbali ya usafiri wa rasilimali watu na bidhaa. Kamati imepitia malengo makuu yaliyowekwa katika maeneo ya reli, barabara, bandari na usafiri anga na kugundua kuwa kwa ujumla Serikali imeshindwa kufikia malengo yake makuu kama ilivyoyaanisha kwenye Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Taifa (2011/12-2015/16). Maeneo mengi yapo chini ya lengo la utekelezaji kwa asilimia 50 na hii imechangiwa sana na kutopatikana fedha kwa wakati au kutopatikana kabisa kwa fedha za kugharamia miradi husika.

**Mheshimiwa Spika**, mfano mzuri ni reli ya kati, lengo la mpango lilikuwa ifikapo mwaka 2015 Serikali itakuwa imekarabati kilometa 2,707 za reli ya kati, lakini mpaka sasa ni kilometa 136 tu za reli ndizo zimekarabatiwa (hatua hii ni asilimia 5.02 tu ya lengo).Aidha, Serikali imekarabati na kununua vitendea kazi kama vile vichwa vya treni, mabehewa na mabehewa ya breki. Vilevile Serikali imeendelea Kukamilisha Uchambuzi yakinifu wa reli ya Musoma-Arusha na Mtwara-Songea-Liganga.

**Mheshimiwa Spika,** sura tuliyoitoa kwenye miradi ya reli ndio tunayoiona kwenye miradi ya nishati, bado hatujafikia lengo la Kuongeza uzalishaji wa umeme kutoka 900 MW (mwaka 2010) hadi 2,780 MW (mwaka 2015); mpaka sasa ni tumefikia kiwango cha 1246 MW tu sawa na asilimia 48.8 ya lengo. Aidha, tunaweza kusema tumejitahidi kufanya vizuri kidogo kwenye miradi ya barabara kwa kujenga kiwango cha lami (kilomita 2,775 sawa na asilimia 53.3) hata hivyo lengo la kujenga Kilomita 5,204 halikufikiwa. Pia, hali si nzuri kwa upande wa miradi ya bandari pamoja na usafiri wa anga.

### 2.2.2 Sekta ya Kilimo

**Mheshimiwa Spika**, lengo kubwa la Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Taifa ilikuwa ni kuongeza ukuaji wa Sekta ya Kilimo kutoka asilimia 2.7 kwa mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 6 kwa mwaka 2015. Hata hivyo, ukuaji wa Sekta ya kilimo mpaka sasa umefikia asilimia 3.4 kwa mwaka 2014 chini ya lengo lililokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa miradi ya sekta ya kilimo ipo nje ya malengo tuliyojiwekea hasa kwa upande wa uzalishaji wa mazao ya thamani, mifugo na uvuvi. Changamoto bado ipo kwenye kuongeza maeneo la umwagiliaji kutoka hekta 330,000 kwa sasa hadi hekta 1,000,000 (mpaka sasa tumefikia hekta 461,326 sawa na asilimia 46.1 ya lengo); usimamizi thabiti wa upotevu wa misitu pamoja na ukuaji wa sekta ya mifugo (ambayo imekua kwa asilimia 1.5 kutoka 1.4 (mwaka 2010) hadi 2.2 (mwaka 2014). Ni dhahiri katika sekta ya mifugo serikali haijaweza kuisimamia vya kutosha na kuona namna gani inasaidia kukuza uchumi wetu ukilinganisha na nchi nyingine kama Ethiopia, sudan na Botswana.

**Mheshimiwa Spika**, sekta ya uvuvi imekua kutoka asilimia 0.9 kwa mwaka 2010 hadi 2.0 kwa mwaka 2015 hii ikiwa ongezeko la asilimia 1.1 Ukuaji huu upo chini ya kiwango kilichowekwa cha asilimia 7 kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa

**Kielelezo namba 6: Ukuaji wa Kilimo na Mchango wake katika Pato la Taifa (GDP) 2010 – 2014**

| Sekta | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Ukuaji Sekta ya Kilimo** | **2.7** | **3.5** | **3.2** | **3.2** | **3.4** |
| Mazao | 3.7 | 4.8 | 4.2 | 3.5 | 4.0 |
| Mifugo | 1.4 | 1.6 | 1.8 | 2.0 | 2.2 |
| Uwindaji na Misitu | 3.4 | 3.3 | 3.5 | 4.7 | 5.1 |
| Uvuvi | 0.9 | 2.6 | 2.6 | 5.5 | 2.0 |
| **Mchango wa Kilimo Katika Pato la Taifa** | **26.3** | **25.6** | **24.8** | **23.8** | **28.9** |

Chanzo : Wizara ya Fedha

### 2.2.3 Sekta ya Viwanda

**Mheshimiwa Spika**, malengo makuu ya Mpango wa Kwanza wa maendeleo yalikuwa ni kuhakikisha kuwa sekta hii inakua kufikia asilimia 11 kwa mwaka ifikapo mwaka 2015/16. Mpaka sasa lengo hili halijaweza kufikiwa, kwani hadi kufikia mwaka 2014, sekta hii imekuwa kwa asilimia 6.8 tu. Kwa upande wa mchango wa kukuza ajira umekuwa chini ya kiwango, mpaka kufikia mwaka 2014 iliajiri watu watu 133,231 nje la lengo la watu 221,000. Aidha, kwa upande wa mauzo ya nje kwa bidhaa za viwandani, sekta hii imefanya vizuri kwa kuvuka lengo la asilimia 19.1 na kufikia asilimia 23.3

### 2.2.4 Sekta ya Madini

**Mheshimiwa Spika**, wastani wa ukuaji wa Sekta ya madini ni wa kuridhisha. sekta hii imekua kwa wastani wa asilimia 6.7. Changamoto kubwa katika sekta hii ni kuhakikisha namna gani tunawajumuisha wachimbaji wadogowadogo kwenye uchangiaji wa pato la Taifa; kuchakata madini hapahapa nchini; mwingiliano wa leseni baina ya wawekezaji wakubwa na wadogo pamoja na kukosekana kwa mitaji kwa wachimbaji wadogo.

### 2.2.5 Maendeleo ya rasilimali watu na huduma za jamii (afya, elimu na maji)

**Mheshimiwa Spika**, ili nchi ifanikiwe katika maendeleo inahitaji kuwa na nguvu kazi ya kutosha yenye uelewa na taaluma mbalimbali inayokidhi mahitaji ya soko na itakayokuwa chachu ya kuleta matokeo thabiti katika sekta husika. Dhana hii ya maendeleo ya rasilimali watu lazima ihakikishe inawajbika katika msingi ya uadilifu na uwajibikaji katika sekta husika. Katika misingi hii napenda kuliaharifu bunge lako tukufu kuwa Serikali imejitahidi sana kuhakikisha maendeleo ya rasilimali watu yameongezeka na hivyo kufikia takribani ya asilimia 70 ya lengo la mpango wa mpango wa kwanza wa maendeleo ya Taifa. mfano mzuri tunauona katika kuongezeka udahili wa vyuo vikuu vya elimu ya juu kutoka wanafunzi 262,376 (mwaka 2010/11) hadi kufikia wanafunzi 362,880 (mwaka 2013/14) na pia ujenzi wa vyuo mbalimbali kama vile kampasi ya Mlonganzila ( chuo Kikuu cha Tiba Muhimbili) na Chuo Kikuu cha Dodoma. Kwa upande wa elimu ya msingi na sekondari kumekuwepo na mafanikio hasa kupunguza idadi ya wanafunzi wanaokatisha masomo.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto ipo kwa upande wa sekta ya afya, huduma za afya zimeimarika ingawa hazijafikia malengo ya Mpango wa Kwanza wa Maendeleo hasa kwa upande wa kupungua kwa idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano kutoka 81 kwa mwaka 2010 hadi vifo 54 mwaka 2013 kwa kila watoto 1000; na vifo vya mama wajawazito kutoka 454 mwaka 2010 hadi 410 mwaka 2014 kwa kila vizazi hai 100,000.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweza kusimamia ipasavyo na kupunguza maambukizi mapya ya magonjwa mbalimbali ikiwemo UKIMWI, Maralia, Kifua Kikuu na Ukoma. Hatua hizi zote zimeiwezesha Tanzania kuvuka malengo ya Milenia. Mwelekeo wetu kwa sasa ni namna gani serikali itajipanga kuweza kuongeza huduma za afya hasa kwa upande wa ujenzi wa zahanati kila kijiji, upatikanaji wa madawa na wauguzi kwenye maeneo husika.


**Mheshimiwa Spika**, kwa upande utekelezaji wa miradi ya Maji, hali sio nzuri kabisa. Kamati imepitia na kuchambua malengo takribani manne tuliyojiwekea kwenye Mpango wa Kwanza wa Maendeleo na kugundua kuwa ni lengo moja la upatinaji wa maji katika wilaya na miji midogo ndio tumeweza kufikia malengo. Malengo mengine kama vile kuongeza idadi ya makazi wenye huduma za maji vijini kuongezeka (kutoka 57.8 hadi 65% mwaka 2015); Idadi ya Makazi katika Mikoa wanaopata huduma ya maji (kutoka 86% mwaka hadi 95% mwaka 2015; na Idadi ya wakazi wa Dar es salaam wanaopata huduma ya maji kuongezeka (kutoa 55% hadi 75% ifikapo mwaka 2015) hayajaweza kufikiwa.

## 2.3 Mapitio ya Sera ya Kuondoa Umaskini

**Mheshimiwa Spika,** kamati ya Bajeti inatambua kuwa mojawapo ya hatua kubwa ya kupiga maendeleo sio tu kukua kiuchumi pia na kuhakikisha umaskini wa kipato kwa wananchi unapungua. Ukifuatilia kwa umakini viashiria vya umaskini yaani; umaskini wa kipato (umaskini wa mahitaji ya msingi), pengo la umaskini; na tofauti ya kipato utagundua kuwa jamii wa watu wanaoishi vijijini ndio inayoathirika zaidi na viashiria hivi vya umaskini. Mfano, takwimu zinaonyesha kuwa umaskini wa msingi **(income poverty)** kwa Dar es Salaam ni asilimia 1.5, maeneo mengine ya mijini ni asilimia 14.4 na maeneo ya vijini ni asilimia 84.1; pengo la umaskini **(poverty gap)** kwa Dar e salam ni asilimia 0.8, maeneo mengine ya mjini ni asilimia 5.5 na vijijini ni asilimia 7.9; na kwa upande wa tofauti ya kipato **(poverty inequalities)** ni kubwa mara nne zaidi ukilinganisha kati ya jamii inayoishi mjini na ile ya vijijini. Kwa takwimu hizi utaona kuwa tafsiri ya dhana ya kukua uchumi umesaidia kupunguza umaskini sio sahihi sana ukizingatia kuwa sekta tunazozitegemea katika kukuza uchumi wetu mathalani mawasiliano, ujenzi na huduma za fedha n.k hazijumuishi idadi

kubwa ya watu na pia shughuli nyingi za sekta hizi zinafanyika katika maeneo ya mjini ambapo kuna idadi ndogo ya watu. Ni wajibu wa Serikali kuhakikisha katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa maendeleo wa Taifa ukuaji wa wa uchumi unabebwa na sekta zinazohusisha idadi kubwa ya watu matahalani kilimo na viwanda ili ukuaji huu uweze kutiririka na kuwafikia wananchi walio wengi vijijini.

**Kielelezo Namba 7: Mwenendo wa kiwango cha umaskini ukilinganisha na Malengo ya MKUKUTA**




**Mheshimiwa Spika**, bado juhudi zinahitajika zaidi kuhakikisha umaskini wa mahitaji ya msingi (kipato) unapungua kutoka kiwango cha asilimia 28.2 na kuweza kufikia malengo ya **MKUKUTA** ambayo ni asilimia 19.3 ambayo pia ni malengo ya millennia **(MDG)**.

## 3.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA BAJETI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MUUNDO WA MPANGO WA PILI WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2016/17- 2020/21)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti imepitia na kuchambua kwa kina mapendekezo ya Muundo wa Mpango wa pili Maendeleo wa Taifa (2016/17-2020/21) unaounganishwa na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umasikini Tanzania (MKUKUTA) ambao una dhana ya kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu (***Nurturing Industrialization for Economic Transformation and Human Development*)**. Kamati inatambua lengo la Mpango huu na ule uliopita ni kuhakikisha Tanzania inakuwa ni nchi yenye Uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025; lakini pamoja na hayo kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

### 3.1. Muundo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti inakubalia na kuunganisha Mpango wa Maendeleo pamoja na MKUKUTA ili kuwianisha agenda ya kupunguza umaskini katika mipango ya maendeleo. Hatua ya kuunganisha itasaidia kutatua changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa MKUKUTA na Mpango kwa pamoja na hivyo kutanzua changamoto za utekelezaji. Aidha, Kamati inakubaliana na Serikali kuhusu kuhusishwa kwa jitihada nyingine ambazo zilikuwepo chini ya Mpango wa Kwanza wa Miaka Mitano kama vile; Matokeo Makubwa Sasa *(Big Result Now)*, Mpango Mama wa Kutathmini Umasikini *(Poverty Monitoring Master Plan)* na Malengo ya Maendeleo Endelevu *(SDG's Sustainable Development Goal)*; kwenye muundo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21).

### 3.2. Ujumuishwaji wa vipaumbele vya Mpango wa Kwanza katika Mpango wa Pili

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti inashauri kuwa ni vema vipaumbele vilivyoainishwa kwenye mpango wa maendeleo uliopita ambavyo havijatekelezwa vikahuishwa kwenye mpango huu mpya ili kuhakikisha kuwa dhana ya ***kufungulia fursa za ukuaji wa uchumi wa Taifa'*** inafungamana na dhana mpya '***kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu'***.

### 3.3 Msingi Mkuu wa ukuaji wa uchumi na kuondoa umaskini

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa ukuaji wa uchumi unaonyesha kuwa unategemea zaidi sekta ya huduma kuliko sekta za uzalishaji kama kilimo na viwanda. Mwenendo huu sio endelevu kuweza kukidhi kuleta maendeleo tarajiwa na kuondoa umaskini wa kipato. Kamati inapendekeza kuwa muundo wa Mpango wa pili wa Maendeleo ujikite zaidi katika sekta ya kilimo na viwanda vinavyochakata mazao ya kilimo pamoja na masoko yake. Uzoefu unaonyesha kuwa Uchumi unaotegemea viwanda (*industrialized economy)* unashamiri pale ambapo sekta ya kilimo inakuwa endelevu na inayojitosheleza.

### 3.4 Upatikanaji wa vyanzo vya Mapato vya kugharamia wa Mpango wa pili.

**a) Sekta Binafsi**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeanisha maeneo na mikakati mbalimbali ikiwemo sekta binafsi kushiriki katika kugharamia wa Mpango wa Pili wa maendeleo. Hata hivyo, bado Sekta binafsi nchini inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo kwa namna moja au nyingine zitaathiri ushiriki wao kikamilifu katika kuchangia mapato ya kugharamia Mpango husika. Kamati inashauri Serikali kufanyia marekebisho maeneo mbalimbali yanayohusu sekta binafsi kama ifuatavyo:-

i) Kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini. (*Doing Bussness and investment climate*). Kwani, Tanzania imekuwa nchi kati ya nafasi ya 128 hadi 131 katika kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo;

ii) Serikali ihakikishe kuwa Sheria zinazosimamia masuala ya uwekezaji zinakuwa thabiti na zisizobadilika mara kwa mara. Kwa mfano kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2009 hadi 2015; Sheria ya Uwekezaji imebadilishwa takribani mara sita, hii inaonyesha kwamba sheria na sera zetu za uwekezaji hazipo thabiti;

iii) Serikali ifanye mapitio ya Sera na Sheria Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2010 (Public Private Partnership Act 2010) ili kupunguza mkanyiko wa usimaizi na ufuatiliaji wa miradi ya PPP ikiwa pamoja na kuanzisha kituo cha usimamizi wa miradi ya ubia;

iv) Serikali ianze kufikiria kujiondoa kwenye utaratibu wa kukopa katika taasisi za fedha na Mabenki ya ndani ambao unasababisha sekta binafsi kukosa mikopo kutoka katika vyanzo vya ndani vya fedha hivyo kuathiri ushiriki wao katika kuimarisha uchumi wa Taifa na kutekeleza ugharamiaji wa miradi ya maendeleo.

**b) Sekta ya Umma**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ndiyo mdau Mkuu katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano, hivyo ni vema ikatatua changamoto zinazoikabili katika ukusanyaji wa mapato ili iweze kugharamikia Mipango ya Maendeleo. Changamoto hizo ni:-

i) Serikali ni lazima iondokane na kutegemea mikopo na misaada kutoka nje na badala yake iimarishe ukusanyaji wa mapato ya ndani kwani ndio chanzo cha uhakika,Mapato yatokayo na Misaada na Mikopo kutoka nje yamekuwa sio chanzo cha uhakika cha kugharamia miradi ya maendeleo; na masharti yake yamekuwa yakibadilika mara kwa mara.

ii) Serikali inatakiwa kuziba mianya yote ya rushwa katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali na kutekeleza kikamilifu Sheria ya uhujumu uchumi *(The Economic and Organaised Crime Control Act of 1983)* ikiwa ni pamoja na kwafilisi wahujumu uchumi;

iii) Serikali ipunguze matumizi ya hati fungani katika kuziba nakisi ya bajeti, Kwani kutokana na ufinyu wa Soko la mitaji mara nyingi wanunuzi wakubwa wa hati fungani ni Mabenki na Taasisi za Fedha zilizopo nchini. Hatua hii hupunguza ukwasi wa ziada *(excess liquidity)* ya Taasisi za Mabenki ambayo ingetumika kutoa mikopo kwa Sekta Binafsi;

iv) Serikali ichukue hatua madhubuti na za makusudi kuhakikisha kwamba Watanzania wanakuwa na utamaduni wa kuweka akiba ili iongeze upatikanaji wa mikopo kwa watu binafsi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo.

### 3.5 Maboresho ya sekta ya miundombinu

**Mheshimiwa Spika,** Katika maeneo ya kipaumbele ya Mpango wa pili wa maendeleo eneo mojawapo lililoainishwa ni sekta ya miundombinu hasa kwa upande wa reli, barabara, bandari na usafiri wa anga. Kamati ya bajeti inashauri kwamba maendeleo ya viwanda yaliyokusudiwa kutekelezwa yazingatie uboreshaji wa miundombinu hasa kwa upande wa upanuzi wa bandari, miradi ya barabara, reli, umeme, na maji

### 3.6 Muda wa kuzingatia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya bajeti inashauri Serikali kuhakikisha kuwa mpango wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo utakaowasilishwa hapo baadae uonyeshe muda na gharama za utekelezaji wa miradi husika. Aidha, Serikali iimarishe vitengo vya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi itakayoainishwa.

### 3.7 Mapendekezo ya jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti inatoa ushauri wa jumla kama ifuatavyo:-

i. Kuhaulisha sheria zote zinazohusiana na masuala ya Uwekezaji nchini. Mfano *Tanzania Investment Act 1997, Export Processing Zone Act 2006 , Mining Act 2010 na Public Procurrement Act, 2011*. Kuhaulishwa kwa sheria hizi kutahamasisha Sekta Binafsi kutoka ndani na nje ya nchi kushiriki katika utekelezaji wa Mpango kwa

sababu taratibu za uwekezaji katika Sekta mbalimbali zitakuwa chini ya mwavuli mmoja.

ii. Kukamilisha Tathmini ya Uwezo wa kukopa na Kulipa (*Credit Rating)* ili kupanua wigo wa Sekta Binafsi na Serikali kukopa kutoka katika vyanzo vya fedha vya nje;

iii. Serikali ihakikishe kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya kulipa fidia na utengenezaji wa miundombinu ya msingi kwenye maeneo mbalimbali ya hasa ile ya miradi mikubwa ya kielelezo (flagship projects) zinapatikana kwa wakati uliopangwa

iv. Serikali ihakikishe upatikanaji wa rasilimali watu wenye ujuzi, uwezo na taaluma ya kufanya kazi katika sekta mbalimbali za uchumi itakayokuwa chachu ya kuleta matokeo thabiti katika sekta husika

v. Serikali iendelee kusimamia suala la uadilifu na uwajibikaji wa watumishi wa sekta ya umma na sekta binafsi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo katika masuala ya ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali.

vi. Serikali ihakikishe kuwa dhamana/hatifungani zitakazouzwa kwenya masoko ya nje lazima ziwe na riba ya kiushindani na fedha zitakazopatikana ni lazima ziwekezwe kwenye miradi ambayo ina tija kwa maendeleo ya Taifa. Kufanya kinyume na hivyo ni kutumbukiza Taifa katika mzigo wa deni lisili himilivu;

vii. *The Debt health Initiative.* Mpango huu unalenga kuelekeza fedha zilizokuwa zitumike kulipa mikopo katika kupambana na magonjwa ya Maleria, UKIMWI na Kifua Kikuu. Tanzania inaweza kutumia mfuko huu kutimiza malengo ya kupamba na magonjwa hayo katika sekta ya afya hata hivyo bado kuna changamoto miundombinu kama vile zahanati na vituo vya afya ambavyo ndio itakuwa nyenzo kuu katika kusimamia mapambano dhidi ya magonjwa hayo.

viii. Serikali ipunguze urasimu katika kutoa maamuzi yatakayoathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye sekta mbalimbali.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kukushuruku kwa mara nyingine kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya

Bunge lako Tukufu. Napenda nimshukuru Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Philip Mpango, Mb na Naibu Waziri Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nawashukuru pia wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili Muundo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2016/17-2020/21.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali yaliyohusu muundo wa mpango husika. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo;

1. Mhe. Hawa A. Ghasia, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Josephat S. Kandege, Mb - M/Kiti
3. Mhe. Hamida Mohamedi Abdallah, Mb
4. Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mb
5. Mhe. Jerome Bwanausi, Mb
6. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
7. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
8. Mhe. Maria Ndila Kangonye, Mb
9. Mhe. Susan Peter Maselle, Mb
10. Mhe. Agustino Manyanda Masele, Mb
11. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
12. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
13. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
14. Mhe. Janet Zebedayo Mbene, Mb
15. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
16. Mhe. Salma Mohamed Mwassa, Mb
17. Mhe. Susana Chogidasi Mgonukulima, Mb
18. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb
19. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
20. Mhe. Ali Hassan Omari, Mb
21. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
22. Mhe. David Ernerst Silinde, Mb

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hii ni mpya na imefanya kazi kwa kujituma na kwa muda mfupi na hatimaye kuweza kukamilisha taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, ninapenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashililah kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri pamoja na Sekretariati ya Idara ya Kamati ya Bajeti kwa kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha, na naunga mkono hoja**.**

Hawa A. Ghasia, Mb
**MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
**29 Januari, 2016**

**MWENYEKITI:** Sasa tunaendelea, hatua inayofuata ni taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Fedha na Mipango, karibu Mheshimiwa. Mheshimiwa Silinde karibu!

**MHE. DAVID E. SILINDE – NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba imekiukwa na kwa kuwa Kanuni ya 64(1) – (4) cha Kanuni zako za Kudumu za Bunge imekiukwa na kwa kuwa kwa mujibu wa Orodha ya Shughuli za leo Bungeni, kwamba tulipokuja hapa Bungeni tulikuwa tunakuja kuwasilisha mpango na huu ni muundo wa Mpango na yenyewe imekiukwa, hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani haitawasilisha maoni yake mpaka pale Serikali itakapotoa Mpango Rasmi humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, lakini huwa napata shida sana kama Mwanasheria, tusipoweza kuzingatia kanuni, hati ikishawekwa mezani na iko kwenye *Order Paper*…

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Tusibishane naongea. Ikishawekwa kwenye *Order Paper* ndio inaruhusu haya matukio kwa mtiririko huu kwa mujibu wa kanuni kufanyika. Huo Mwongozo ulioombwa, ndio maana kwa heshima zote nikasema, alichokisema Mheshimiwa Zitto ukaongezea sauti yako kwake, nikasema, kichwa hiki kinahitaji kiwe *exercised properly,* nimekubali hiyo. Sasa nikasema ni vema *statement* yenu ikawasilishwa tu maana ipo mezani.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima zote, hasa kwa upande wangu wa kushoto ukishawasilisha kitu mezani na kikapokelewa kiko sahihi mpaka wewe mwenyewe uombe kiwe *withdrawn* kwa utaratibu huo. Sasa huwezi ukafika tu hapa unaanza kusema mpaka uletewe kitu fulani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaenda vizuri tu, lakini nawaombeni sana na ninyi tujaribu kujenga *jurisprudence* ya matumizi ya Kanuni za Bunge. Kwa

maana hiyo, maana Kamati ya Kanuni ya Bunge ipo, mimi nilikuwa nasema twende vizuri tu na suala hili na nisingemlazimisha mtu, kama Kambi ya Upinzani mnajisikia kwamba, hamko tayari kuisoma hotuba hiyo kwa sasa tusingependa tuendeleze malumbano ambayo nayaona hayana tija.

Sasa hivi nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi jioni.

*(Hapa Mbunge Fulani alikuwa akimwelekeza Mwenyekiti nini cha kufanya baada ya kuahirisha Bunge)*

**MWENYEKITI:** Huwezi kutu-*direct* cha kwenda kufanya, tutajulishana. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Wameshasaini hao!

**MBUNGE FULANI:** Wameshasaini hao!

**MBUNGE FULANI:** Wewe mjinga kelele!

**MBUNGE FULANI:** Fedha za baba yako?

**MBUNGE FULANI:** Fedha za baba yako hizi?

*(Saa 6.16 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Waheshimiwa Wabunge, asubuhi nilikuwa nimeombwa Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) wakitaka kiti kitoe Mwongozo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kuhusiana na hoja ambayo imewasilishwa asubuhi hii na Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, ili twende pamoja na wale mlio na Katiba ya Jamhuri ya Muungano, kwa sababu yalitolewa madai mazito kidogo, kwamba uwasilishwaji wa hoja hiyo ni ukiukwaji wa Katiba ya nchi kupitia ibara hiyo ya 63(3)(c). Ibara hiyo 63(3), inasomeka hivi: "Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake, Bunge laweza (c) kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano na kutunga Sheria ya Kusimamia Utekelezaji wa Mpango huo."

Kwa hiyo, hoja ilikuwa ni hiyo, Katiba inatuongoza hatuwezi kukiuka. Pili, sheria yenyewe iko wapi inayoendana na Mpango huo na Mpango wenyewe

uko wapi, ndiyo ilikuwa hoja hiyo. Sasa kutokana na uzito wa suala hili ndiyo maana nilisema nilichukue nami nikalitafakari vizuri ili ninapokuja kutoa toka Mwongozo uwe umetokana na *an informed position.*

Nimefanya hivyo, nimelitafakari sana suala hili na baada ya kutafakari niseme wazi kabisa kwamba hakuna ukiukwaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Kilicholetwa na Serikali, ni mchakato wa kuwashirikisha wawakilishi wa wananchi wa Tanzania ili watoe maoni, ushauri na mapendekezo yao kuhusiana na Mpango unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Waheshimiwa Wabunge, kitu ambacho sote lazima tukubali, Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa kanuni ya 94(1), Bunge linapofanya kazi hiyo huwa haliketi kama Bunge, linaketi kama Kamati ya Mipango. Nadhani hiyo ndiyo dosari ambayo tunaweza tukaiona kwamba, Kamati ya Mipango ni Kamati, tunakaa kama Bunge zima, lakini hii inaitwa hivyo kwa sababu tunashughulika na mipango na hapa ilikuwa Mpango huo wa muda mfupi na ndiyo mana Katiba inasema: "…au wa muda mfupi" na Ibara ya 63 wala haisemi ni lini ilete huo Mpango, inapoleta sasa lazima tuangalie ni nini kinachotakiwa kifanyike.

Mpango wetu huu unaomalizika tarehe 30 Juni, 2016, miaka mitano ya awamu ya kwanza, ulianza na *process* hiyo ya kuletwa Bungeni na tunapoanza sasa hatua ya kwanza, Mpango wa Pili, lazima na Bunge lenyewe lipewe nafasi ya kulisemea ili liamue. Bunge linapoamua huwa linaamua kama Bunge kupitia hoja na hitimisho la hoja hiyo ya mapendekezo ya Mpango huu wa mwaka mmoja mfupi na ule mwingine wa miaka mitano ambao huu mfupi unatokana na huu wa miaka mitano, hitimisho lake litakuwa ni siku ambayo Serikali kupitia Waziri wa Fedha na mwenye dhamana ya Mipango atakaposoma Mpango wa Serikali kwa mwaka unaofuata wa fedha na jioni Waziri wa Fedha anaposoma Bajeti ya Serikali kwa mwaka unaofuata.

Kwa hiyo, *the annuality,* ule mwaka mwaka wa Mpango ambao ndiyo tuliokuwa tunatumia, ambayo ndiyo kanuni ya 94, inapaswa izingatiwe, ndiyo imekaa katika sura hiyo.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka Bunge halikuweza kukutana mwezi Oktoba/Novemba kama Kanuni ya 94(1) inavyotaka kwa sababu tulikuwa na shughuli kubwa ya uchaguzi ambayo imewezesha ninyi viongozi kuwa hapa kutoka kwa wananchi, *mandate* mpya ya Serikali ya Awamu ya Tano na Bunge la Kumi na Moja.

Sasa Serikali na Bunge hatukuwa na njia nyingine, kwa hiyo ndiyo maana lazima mchakato huu ufanyike sasa, ili mwezi wa tatu kwa mujibu wa Kanuni ya

97(1), tunatakiwa tarehe10 au 11, kama tarehe 10 siyo siku ya kazi, tarehe 11, Serikali iwasilishe mbele ya Wabunge na kwa mazoea ya nyuma, mwaka jana hili lilifanyika pale kwenye Ukumbi wa Mwalimu Nyerere, Dar es Salaam.

Waziri mwenye dhamana ya Mipango anawasilisha Mpango, Waziri wa Fedha anatoa ile *statement* ya ukomo wa bajeti *(budget frame),* wakishawasilisha, Katibu wa Bunge ndiye anazipeleka kwa Spika ili Spika sasa aelekeze zipelekwe kwenye Kamati ya Bajeti hadi watakapokuja kutoa taarifa kwa niaba ya Bunge hiyo siku ambapo Serikali itakapowasilisha Mpango na Bajeti ya Serikali.

Kwa mujibu wa Kanuni zetu, hiyo siku ya kusomwa kwa Bajeti ya Serikali, mnaanza asubuhi, Waziri mwenye dhamana ya Mipango anawasilisha hoja yake ya Mpango, utekelezaji wa hali ya mwaka jana, lakini na mwaka unaofuata, jioni sasa Waziri wa fedha anatoa hoja kuhusiana na Bajeti ya Serikali. Kwa hiyo, tunakuwa na hoja mbili, lakini huwa zinajadiliwa kwa pamoja, hoja ya Mpango na hoja ya Bajeti ya Serikali. Sasa utaratibu wa kuziamua kwa upande wa hoja ya bajeti tunafahamu, jina moja baada ya lingine linasomwa useme msimamo wako ni ndiyo au hapana.

Sasa haya ndiyo yanapaswa yafanyike, sasa nachukua muda kulieleza hili kwa sababu nawasihi sana tukazisome kanuni, maana tukishaelewa kwa utaratibu ule wa mpango wa mwaka mmoja, uko *very clear* ndiyo 94 ile, lakini ule Mpango mkubwa sasa, hiyo ndiyo ilikuwa hoja ya wenzetu kwamba uko wapi? Sasa hilo na baada ya tafakari yangu nimeona kwamba ule Mpango haupo. *(Makofi)*

Tunachotakiwa kufanya kwa sababu ni sehemu ya maamuzi, najua Serikali itajipanga tu, lakini sisi kama Bunge, ingependeza kama Serikali ingetuletea na ule Mpango, ile Rasimu waliyonayo, tukatoa mapendekezo yetu sasa kama wanaweza, siwezi kuwalazimisha. Nasema ingependeza kama ingekuwa hivyo ili mwezi wa tatu ule Mpango wa mwaka mmoja, 2016/2017 na ule Mpango wa miaka mitano ukawasilishwa pamoja ili sasa siku ya Bajeti, Mpango utawasilishwa wa mwaka mmoja lakini pia ule Mpango wa miaka mitano ili sasa mnapochangia Wabunge na kuja kuhojiwa mnajua mmefanya marekebisho kiasi gani, mnashauri nini na mnaona mchakato wa kuishauri Serikali, ni maeneo yapi ambayo yamezingatiwa na Serikali.

Nimeona niyaseme haya kwa sababu nilishtuka sana, suala la kukiuka Katiba ni hoja nzito sana, lakini kitu ambacho kimetokea ni kughafilika tu kwamba badala ya kukaa kama Kamati ya Mipango tumekaa kama Bunge. Kwa vile tunaongozwa pia na kanuni, Kanuni inasema tukio hili mtalifanya mwezi Oktoba/Novemba huwezi tu ukasimama hapa na kufanya, lazima hoja itolewe kuruhusu kutengua Kanuni hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tukienda hivyo tutakuwa tunakwenda vizuri na kwa maana hiyo njia nzuri ya kutufikisha ili tuweze kuketi kama Kamati ya Mipango mtoe ushauri na mapendekezo yenu kwa Mpango huo 2016/2017 ni kuruhusu tuketi kama Kamati ya Mipango. Lini hilo lifanyike itategemea utayari wa Serikali, *how ready*, lakini siwezi kuisemea Serikali, ila niko hapa ku-*guide* na kusimamia Kanuni, ili hoja hii iliyo mbele yetu, maana siwezi tu kuwaambieni hoja haipo hapana, hoja ipo, hata kama ilikosewa kufika hapa, nikamwita mtoa hoja lazima nizingatie kanuni, si ndiyo!

Kwa hiyo, naishauri Serikali kupitia Kanuni ya 58(5) ambayo inaruhusu kwa hoja ambayo haijaamuliwa inaweza ikaondolewa kwa idhini ya Bunge. Hiyo ndiyo njia sahihi, iliyo nyoofu, inayozingatia Katiba na pia Kanuni za Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini narudia, hatujakiuka Katiba hata kidogo, ushirikishwaji wa wawakilishi ninyi katika kutoa ushauri ndiyo lazima uje katika sura hiyo.

Sasa nimwite mwenye hoja, yaani Waziri wa Fedha na Mipango, atekeleze hilo jukumu ili yeye aitoe ile hoja yake kwamba anaomba idhini ya Bunge, halafu niwahoji. Mheshimiwa mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri uje mbele hapa.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maelezo uliyoyatoa na kwa kutumia Kanuni ya 58(5)ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba ruhusa ya kuondoa hoja niliyoiwasilisha leo asubuhi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kwa Kipindi cha miaka mitano 2016/2017 mpaka 2020/2021 *(The Framework of the Second Five Years Development Plan 2016/2017 to 2020/2021). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Walioafiki wameshinda. Kwa hiyo, hoja iliyo mbele yetu imeondolewa rasmi.

Baada ya kusema hayo, nina tangazo, pale kwenye mashine za ukaguzi iwe ni hapa au kule, lakini Mheshimiwa Waitara, Mbunge wetu wa Ukonga anasema mfuko alionao siyo wa kwake. Kwa hiyo, anaomba sana yule

aliyechukua mfuko ambao kuna *contents* siyo za kwake awasiliane naye. Bahati mbaya hakuandika simu yake hapa, lakini naelewa adha aliyonayo sasa hivi, lakini naamini hata yule mwenzake aliyechukua kama naye alikuwa na *documents* zake.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kazi nzuri mliyofanya, nifanye kazi moja tu kubwa ya Kikanuni, nayo ni kuliahirisha Bunge hadi siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 10.21 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 1 Februari, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*